TRUTH CENTERED TRANSFORMATION

MODULE 1



UTANGULIZI KWA HUDUMA KAMILIFU

MWONGOZO WA MWALIMU

Mabadiliko yaliyojikita katika ukweli ni utume wa Reconciled World habarika zaidi kwenye tctprogram.org

Reconciled World

Mabadiliko yaliyojikita katika ukweli - Moduli 1: Utangulizi kwa huduma kamilifu (toleo la 4) Hakimiliki ©2012 Reconciled World, Phoenix, Arizona, United States of America. www.reconciledworld.org

Kazi hii imeandaliwa kwa kuzingatia masharti ya leseni ya the Creative Commons Attribution-ShareAlike 3.0 . Unaruhusiwa na kutiwa moyo kutumia kazi hii, kunakili, kusambaza, na kutangaza kwa masharti yafuatayo:

Nukuu – Lazima unukuu kazi hii kwa kutoa maelezo haya: Hakimiliki © 2012. Imechapwa na Reconciled World (www.reconciledworld.org) kwa masharti ya leseni ya the Creative Commons Attribution-ShareAlike 3.0. kwa habari zaidi, ona www.creativecommons.org.

Siyo ya kibiashara – Huwezi kutumia kazi kwa malengo ya kiabiashara.

Kama unapenda kutafsiri kazi hii, tafadhali wasiliana na info@tctprogram.org.

Nukuu zote za maandiko matakatifu, isipokuwa yameonyeshwa vinginevyo, yamechukuliwa kutoka kwenye Biblia takatifu, toleo la New International®, NIV®. Hakimiliki ©1973, 1978, 1984, 2011 ya Biblica, Inc.TM ikitumika kwa ridhaa ya Zondervan. Haki zote zimehifadhiwa dunia nzima. www.zondervan.com "NIV" na "New International Version" ni alama za biashara zilizosajiliwa United States Patent and Trademark Office na Biblica, Inc.TM

Shukrani

Kuna namna ndogo ya kumshukuru kila mmoja ambaye amechangia katika yote yaliyomo kwenye kazi hii na kufanya programu hii iwe kama ilivyo. Sehemu kubwa ya msukumo wa mwanzo ulitokana na mafundisho ya Darrow Miller wa Disciple Nations Alliance na Bob Moffitt wa Harvest Foundation. Programu hii imeanza na kutekelezwa katika miaka yangu kadhaa nikiwa na shirika la Chakula kwa wenye njaa. Ninawashukuru kwa kunipa nafasi ya kujaribu mawazo haya na hata kutoa fedha kufanya majaribio haya yawezekane.

Katika moduli hii ya kwanza, nimetumia sana matirio kutoka kwenye vitabu vya Bob na Darrow hasa kutoka "Development Ethic" cha Darrow Miller na "Leadership Development Training Program" cha Bob Moffitt. Baadhi ya mawazo ya namna ya utoaji maarifa nayo yametoka kwa Mark Wilson. Hadithi ya Kuvuka Mto katika somo la 8 si yangu, kama inavyoonekana katika matirio mengi kwamba nimeshindwa kumpata mwandishi wake wa mwanzo.

Ninawashukuru muno wote ambao nimefanya nao kazi kwa miaka waliosoma na kuweka katika utekelezaji mawazo haya. Ni mashujaa wangu. Ni utumiaji wao na mrejesho wao vimefanya kazi hii iwezekane, na kunitia moyo kumenifanya niendelee hata pale ambapo nilikaribia kukata tamaa. Bado nina nafasi ya pekee ya upendo kwa timu ya kwanza ya wakufunzi waliokaa katika hali ya kuchanganyikiwa nilipojifunza namna ya kufundisha na kitu cha kufundisha. Walijaribu kwa uvumilivu kuelewa na hata kufundisha mawazo ambayo baadaye tulitambua yalikuwa magumu sana kwa mazingira yao. Na bado Mungu alitoa jamii hizo katika umasikini. Kumbusho lisilo na mwisho kwamba hii kamwe haikuwa kuhusu mimi au nilichokuwa nafanya, bali kuhusu Mungu na alichokuwa anafanya. Ninaguswa kwa kiasi kisichokuwa na kipimo kwamba Mungu ameniruhusu niwe sehemu ya hadithi hii na kunitumia pamoja na madhaifu yangu yote. Utukufu na uwe kwake tu.

Mwisho, Nataka kumshukuru Mume wangu aliyeacha utume wake kufanya kazi na mimi katika program hii. Bila yeye Hakuna chochote kati ya hivi kingewezekana. Natambua majitoleo yako mengi uliyofanya kufanya hiki kitokee. Wewe ni upepo chini ya mabawa yangu na nakupenda.

Anna Ho
Executive Director

Kabla ya kuanza

Kujiandaa kufundisha somo

1. Soma **mwongozo wa mwalimu** kwa uangalifu, mara nyingi iwezekanavyo. Weka alama au andika notisi chini ya mstari kujikumbusha pointi za muhimu.
2. Angalia malengo ya kila somo ili ujue mwanafunzi anahitaji kujifunza nini katika somo.
3. Soma aya za **maandiko matakatifu** hapo mbele.
4. Angalia kuona ni matirio gani yanahitajika kwa kila somo na hakikisha unatengeneza nakala ya miongozo ya wanafunzi (handouts) na tengeza picha za kujifunzia zinazotumika kwenye somo.
5. Hakikisha unaelewa kila **kitendo** katika somo (maigizo, michezo, picha za kujifunzia/vionyesh). Unaweza kuifanyia mazoezi na ndugu na marafiki.
6. Pata muda wa **kusali** ili Mungu awaandae wanafunzi, ili wanafunzi wasikie kile Mungu anachotaka wasikie na ili akusaidie kufundisha matirio. Kumbuka ni kwa njia ya Mungu tu kwamba tutawaona watu wakibadilika

Vidokezo kwa ufundishaji wenye tija

1. Fika mapema na andaa materio na sehemu utakayokuwa unatumia.
2. Usipitie materio haraka. Andaa muda wakutosha kwa ajili ya majidiliano, vitendo na mapumziko. Lengo ni kwa watu kuwa na muda wa kuelewa na kushiriki katika mchakato wa kujifunza. Nenda kutoka mada hadi mada kwa spidi ambayo itahakikisha kila mmoja ameelewa. Moduli nyingine zaweza kuchukua nusu siku au siku nzima Zaidi.
3. Fanya marudio mara nyingi. Mwanzoni mwa kila kipindi rudia yale yaliyokwisha fundishwa hadi muda huo. Marudio humsaida mwanafunzi kukumbuka alichojifunza.
4. Fuata mwongozo wa mwalimu na notisi za maandalio.
5. Usisahau kujumuisha sehemu zote nne za kila somo.
    a. Tambulisha mada – vitendo vitaunganisha mada na uzoefu wake wa siku za nyuma.
    b. Toa habari mpya – Kuna njia nyingi za kushirikisha habari mpya.
    c. Wape wanafunzi kitu cha kufanyia kile walichojifunza – kazi huwapa uelewa bora Zaidi kwa kufanya kazi na watu wengine, kufanya kitu au kutumia taarifa mpya kwa namna Fulani.
    d. Husianisha taarifa na Maisha yao – hii ni hatua ya utumikaji ambayo humsaidia mwanafunzi kuamua njia mahususi watakazotumia taarifa waliyojifunza katika Maisha yao. Kujifunza bila kutumia ulichojifunza hakuleti mabadiliko na hakufai.
6. Pitia kanuni za elimu ya watu wazima na maarifa mengine yanayofundishwa katika mafunzo ya kumwendeleza mwezeshaji.
    a. Toa maelekezo bayana
    b. Uliza maswali mengi yenye majibu marefu
    c. Washukuru watu kwa ushiriki wao.
    d. Usiwaambie watu wanachoweza kujifunza vizuri Zaidi kwa kugundua.
    e. Jenga kwenye kitu watu wanachokijua na tambua uzoefu
    f. uwe mvumilivu na usubiri watu wajibu.

7. Mtie moyo kila mmoja kushiriki, akishirikisha na kuchangia katika mijadala. Tafuta namna ya kuwahimiza watu wenye aibu kushiriki bila kuwaaibisha.
8. Sali siku nzima kwa Mungu akuonyeshe na kuwaonyesha wanafunzi mambo mapya

Namna ya kutumia mwongozo huu wa mwalimu

1. **Malengo na Matirio:** Kila somo linaanza na sehemu.
    a. **Malengo** – Wanafunzi waweze kufanikisha haya ifikapo mwishoni mwa kipindi. Ni vizuri kujiuliza kama malengo haya yametimizwa baada ya kuongoza kipindi. Uchukue muda wa kurudia mara kwa mara mada za msingi kuwasaidia kukumbuka.
    b. **Matirio/nyenzo** – Matirio maaalumu yameorodheshwa kwa kila somo ikiwa ni pamoja na picha za kufundishia, vitini (handouts). Unaweza kuchagua kutoa nakala za mwongozo wa mwanafunzi kwa kila mshiriki, au tengeneza idadi ndogo ya nakala kama inavyopendekezwa kwa kila somo. Tunashauri pia kuwa na karatasi ya manila, ubao mweupe, au ubao wa chaki wa kutumia kwa ajili ya kikundi kikubwa.
    c. Mwongozo huu wa Mwalimu utaonesha wakati gani utumie vitu hivi:
        i. Miongozo ya mwanafunzi – utaona alama upande wa kulia wa ukurasa kama hivi pale mwongozo wa mwanafunzi unapohitajika kutumika.
        ii. Vioneshi – utaona alama upande wa kushoto wa ukurasa kama hivi pale kioneshi kinapohitajika kutumika.
2. **Maelekezo kwa mwalimu:** Kuna maelekezo maalum katika somo kukusaidia uongoze mafunzo vizuri. Haya hayakusudiwi kutolewa kwa wanafunzi. Soma haya kabla ili ujiandae kuongoza majadiliano na shughuli. Baadhi ya maswali yatakuwa na majibu yaliyoitalikiwa (italicized) kukusaidia kwama mwezeshaji ujue nini cha kuchota kutoka kwa wanafunzi. Haya si majibu mazuri pekee, bali ni baadhi ya majibu mazuri.
3. **Kutawala muda na mtiririko:** Vipindi vya muda havijawekwa kwa kila somo.
    a. Chukua muda mwingi kadri itakavyohitajika kusaidia watu wajifunze vitu katika somo. Ni bora kuzingatia kitu watu wanachojifunza kuliko kuzingatia kumaliza kipindi katika muda uliopangwa.
    b. Kumbuka kutenga muda kwa wawezeshaji kuanza na ibada, kutoa shuhuda, kujadili matatizo yoyote waliyonayo, na kusali pamoja.

Somo la 1: Hadithi nzima

Malengo

1. Mpango wa Mungu si tu kuona nafsi zikiokolewa bali pia kuona upatanisho wa mahusiano matatu yaliyovunjika kutokana na anguko – uhusiano wetu na Mungu, uhusiano baina yetu wanadamu na uhusiano baina yetu na uumbaji wa Mungu

Nyenzo

1. Picha za kufundishia –
   a. Mahusiano matatu (Picha nne: uumbaji, anguko, upatanisho, Kurudi)
   b. Igizo la Adamu na Eva (nakala mbili)

Utangulizi

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

- Kwa nini Yesu alikufa?

Maelekezo kwa mwezeshaji: Watie moyo washiriki kutoa majibu mengi kadri wawezavyo. Wakumbushe wawezeshwaji/wanafunzi kuwa hakuna jibu la moja kwa moja lililosahihi". Kubali majibu yote kwa kuwa ni sahihi.

Kwa kawaida tunasema Yesu alikuja kutukomboa kutoka kwenye dhambi zetu. Hii ni kweli, lakini alikuja kufanya mengi zaidi ya hilo. Kifo chake msalabani ni sehemu moja tu ya hadithi nzima. Kuuelewa vizuri ujumbe wa Biblia, tunahitaji kuelewa hadithi nzima tangu mwanzo hadi.

Uumbaji

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Kutokana na unachokijua kuhusa namna Mungu alivyouumba Ulimwengu, unawezaje kujibu maswali haya?

- Kulikuwa na uhusiano wa namna gani kati ya Adamu na Mungu? (Mwanzo 1:26-27, 31)
- Kulikuwa na uhusiano wa namna gani kati ya Adamu na Eva? Unadhani walibishana sana? (Mwanzo 2:23-25)
- Kulikuwa na uhusiano wa namna gani kati ya Adamu na uumbaji/mazingira? Je, Adamu alikuwa na vyote alivyohitaji? Je, Alikuwa na chakula cha kutosha? (Mwanzo 1:29-30)

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Onyesha picha namba 1:* ***Uumbaji*** *na uwasaidie wanafunzi kuona kwamba mwanzoni kabla ya anguko kila kimoja katika mahusino haya matatu kilikuwa kikamilifu.*

Anguko

Soma Mwanzo 3:1-20.

IGIZO

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Omba watu wawili kufanya igizo lifuatalo. Wape watu hawa wawili waliojitolea kitini cha igizo*

"Mazungumzo kati ya Adamu na Eva"

Adamu: (akiwa bustanini) Eva, Kufanya kazi bustanini hakika kumekuwa kugumu sana baada ya kumuudhi Mungu kwa kula tunda lile!

Eva: Ndiyo, na hata vijana wetu hawaelewani tena vizuri. Wanabishana na kupigana muda wote. Natumaini hali haitakuwa mbaya zaidi! Na haya majani ya kipumbavu ya mti wa mfigi ninayotakiwa kuvaa. Ni mabaya sana!

Adamu: (Wakibishana) Hata hivyo, hatuna uwezo wa kununua nguo mpya, hivyo usilalamike!
(Kimya) Nimezikumbuka siku hizo, wakati Mungu alipotembea nasi na kuongea nasi. Sasa anasikitika kwamba hata tupo hapa. Na kumbuka jinsi wanyama walivyokuwa wanatutii? Sasa wanakimbia kwa kutuogopa!

Eva: Ndiyo, au wanajaribu kutung'ata! Uuh…Namchukia nyoka! Siwezi kuamini nilipata ushauri kutoka kwa nyoka! vurugu yote hii ni kosa la nyoka!

Adamu: Hapana, nikosa lako! Kamwe huwa hufanyi kitu sahihi! Kwa nini nilifuata ushauri kutoka kwa mtu aliyepata ushauri kutoka kwa nyoka?

Eva: Ah, Usinilaumu. Ni kosa lako! (Akinyamaza, kwa huzuni) Samahani. Haisaidii kupigiana kelele. Adamu, Unadhani ipo siku mambo yatakuja kuwa kama yalivyokuwa awali?

Adamu: Sijui. Mungu pekee anaweza kurekebisha vurugu hii!

Eva: Eeh, hapana - nini sasa? (kelele zinasikika, Anakimbia nje) Acheni kupigana nyie vijana! Acheni sasa hivi. Mnanisikia? Nitamwambia baba yenu, na hatafurahishwa!

Adamu: (Akirudi bustanini, akishusha pumzi) kazi, kazi, kazi, kazi, kazi, kazi,…

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Kutokana na igizo na ulichokisoma katika biblia, ni changamoto gani watu wazozipitia kwa sasa kutokana na anguko?

- Soma Mwanzo 3:8 na 10 – Nini kilitokea wakati wa anguko kwa uhusiano wa mwanadamu na Mungu?
- Soma Mwanzo 3:12 – Nini kilitokea wakati wa anguko kwa uhusiano kati mwanadamu na mwanadamu?
- Soma Mwanzo 3:15 – Nini kilitokea wakati wa anguko katika uhusiano kati mwanadamu na uumbaji?

Baada ya anguko, uovu uliingia duniani; sio tu uovu wa kimaadili, lakini uovu wa kimwili pia. Kabla ya anguko, kulikuwa na chakula cha kutosha na hakukuwa na matetemeko ya ardhi, hakukuwa na mafuriko wala ukame. Kutokana na anguko, sasa tuna vitu vyote hivi.

Anguko liliharibu mahusiano yote matatu.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *onyesha picha ya 2:* ***Anguko*** *na uwasaidie wanafunzi kuona kwamba Anguko liliharibu kila moja ya mahusiano haya.*

Misheni/Utume

Hatua inayofuata ya hadithi kati Mungu na uumbaji wake inapatikana kati ya maelezo ya anguko na mwisho wa agano la kale.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Lionyeshe darasa sehemu kubwa ya kile unachokiongelea katika biblia.*

Hii ni hatua ambapo Mungu anatafuta watu wake. Ana hamu ya kurekebisha kile kilichovunjika.

IBRAHIMU – Soma Mwanzo 12:1-3. Katika sehemu hii Mungu anamwinua Ibrahimu na kumbariki. Kwa nini anambariki Ibrahimu? (*Mungu anataka kubariki mataifa.)* Katika aya hii moja, tunaona mpango wa Mungu kuukomboa ulimwengu mzima. Kupitia kanisa anataka kuleta baraka kwa mataifa.

MUSA – Mungu aliupa ulimwengu amri 10 ili tuweze kujua namna ya kurekebisha mahusiano yaliyovunjika.

- Je, sheria inahusu mambo ya kiroho tu au pia inahusu mahusiano kati yetu sisi wenyewe na sisi na asili?

Amri nne za mwanzo zinarejesha uhusiano wetu na Mungu. Je, amri sita za mwisho zinarejesha uhusiano gani? (*uhusiano baina yetu*). Sheria nzima inahusu uhusiano wetu na Mungu (Kut. 21:3), uhusiano baina yetu (mfano. Kut 21:12), na pia uhusiano wetu na uumbaji (Kut 23:10-12). Zipo sheria mahususi za kusaidia watu wabaki wenye afya (mf. Walawi 13) na kuonyesha jinsi ya kuchukuliana (Mf. Kut 23:1-9). Mungu hajali tu mambo ya kiroho. Anajali maeneo yote ya Maisha yetu. Ndiyo maana alitengeneza sheria kwa kila eneo lililoharibiwa na dhambi.

Soma Kumb. 28:1-14.

- Mungu anasema nini yatakuwa ni matokeo kama watu wake watatii amri hizi?
- Je, baraka anazoahidi Mungu ni kwa mambo ya kiroho tu au ni baraka kwa maisha yao ya kimwili pia?

Mungu aliwainua wafalme na mitume, lakini tena na tena lakini Israeli iliteseka kwa umaskini na vita kwa sababu walikengeuka wakampa Mungu mgongo na na kuacha kuzifuata amri zake.

Soma: 2 Mambo ya Nyakati 7:14

- Mungu anawataka nani wajinyenyekeze na kusali? (*Si watu wote, lakini watu wake wote ambao leo wanaitwa Wakristo*)
- Mungu alisema nini kingetokea kama wangekuwa watiifu? (*Mungu ataponya ardhi yetu*) Hii bado ni kweli hata leo. Haimaanishi kuwa tutaona maisha yakiokolewa. Aya hii inatuambia kwamba Mungu ataleta uponyaji kwa maeneo yote matatu ya mahusiano – mahusiano yetu na Mungu, baina yetu wanadamu na baina yetu na uumbaji.

Msalaba

Hii sio tu ni sehemu nzuri sana ya hadithi, lakini pia sehemu muhimu sana. Katika dini nyingi, watu wanatakiwa kutoa sadaka kuwafurahisha miungu. Katika ukristo, Mungu aliupenda sana ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee afe kwa ajili yetu (ulimwengu).

Soma Wakolosai 1:19-20. Kwa nini Yesu anakufa?

- *Alikufa ili kupatanisha mahusiano yote.*

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Onyesha picha ya 3:* ***Upatanisho****, na ulieleze darasa kwamba Mungu alikuja kupatanisha kila kitu kilichovunjika katika anguko. Hata hivyo, kila kitu hakitakuwa sawa kikamilifu hadi mwisho wa hadithi.*

Yesu alituachia jukumu kubwa (wito mkuu). Tunawajibika sio tu kuwafanya watu wawe wakristo, lakini pia kuyafuasa mataifa. Kuyafuasa mataifa maana yake ni kuyasaidia mataifa yafuate madhumuni ya Mungu katika maeneo yote ambayo Yesu alikuja kupatanisha.

Kurudi

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Soma Ufunuo 21:1-7

- Mwishowe, Uhusiano wa mwanadamu na Mungu unakwenda kuwa wa namna gani?
- Uhusiano kati mtu na mtu unakwenda kuwa wa namna gani?
- Uhusiano wa mwanadamu na viumbe vingine unakwenda kuwa wa namna gani? Tutakuwa na chakula cha kutosha? Tutaugua?

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Onyesha picha ya 4: Kurudi, na wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu akirudi mahusiano yetu yote yatarejeshwa kuwa jinsi Mungu alivyokusudia yawe tangu mwanzo*

Hitimisho

Hii ni hadithi nzima—hadithi nzuri sana kutoka mwanzo hadi mwisho, ya namna Mungu alivyoumba ulimwengu mkalifu; ya namna dhambi ilivyoingia ulimwenguni na kuharibu uhusiano wet una Mungu; ya namna Mungu alivyotupenda sana hata akamtoa mwanae wa pekee ili kuleta upatanisho wa mahusiano yaliyovunjika katika anguko; ya namna Mungu atakavyokuja tena siku moja na kufanya mambo yote kuwa mapya.

Mungu anakupenda sana. Alimtuma mwanaye afe ili uweze kuwa na uhusiano mzuri na yeye, na ili uweze kuwa na mahusiano mazuri na watu wengine na ili uweze kuwa na uhusiano mzuri na uumbaji.

Somo la 2: Wanadamu ni muhimu kwa Mungu

Wazo Kuu

Watu wote wameumbwa kwa sura ya Mungu na ni wa thamani kwake. Twatakiwa kuchukuliana, hata kwa wale ambao hudharauliwa sana, kana kwamba ni viumbe vya thamani vya Mungu.

Nyenzo

1. Mwongozo wa mwanafunzi (SIO LAZIMA):
    a. Kuumbwa kwa mfano wa Mungu (nakala moja kila kikundi)

Utangulizi

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Katika nchi ya Congo, idadi kubwa ya makanisa yameanza kuwafikia wanaojiuza miili yao (umalaya), kwa kuwaruhusu kuishi katika majengo ya kanisa na kuwafundisha ushonaji. Malaya hawa walikuwa ni wasichana waliokuwa wakiishi mitaani kwa sababu walipata ujauzito kabla ya kuolewa na kwa hiyo familia zao ziliwafukuza kutoka nyumbani kwao.

- Je, unadhani hili ni kundi zuri kwa ajili ya kusaidiwa na kanisa?
- Je, kuna makundi ya watu wengine ambao unadhani makanisa yangewaangalia zaidi kuliko hawa Malaya?

Kuumbwa kwa sura ya Mungu

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO AU KIKUBWA

Soma Mwanzo 1:26-27

- watu wanatofautianaje na viumbe wengine? Mungu alitumia nini kama mfano wake kwa wanadamu?
- Ni tabia gani za Mungu zinazoweza kuonekana kwa mwanadamu? Ainisha nyingi kadri iwezekanavyo.

Soma Zaburi 139:13-16

- Aya hii inatuambia nini kuhusu umuhimu wa wanadamu?
- Unadhani aya hii inawahusu watu fulani tu au watu wote?

Mungu alituumba, tumeumbwa kwa uangalifu sana, na ameandika siku zote za maisha yetu katika kitabu. Hatukutokea tu, lakini Mungu amemtengeneza kila mmoja wetu.

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Soma Yohana 3:16

- Mungu alifanya nini kurekebisha ulimwengu?
- Je, Mungu alikufa kwa ajili yetu kwasababu tulikuwa wema? (*Kama hawana uhakika tazama Warumi 5:8.)*
- Kama Mungu alikuwa radhi kumtuma mwanawe afe kwa ajili ya watu, je Mungu anawaona watu ni wa muhimu kiasi gani?
- Hii inaamaanisha nini kwa namna tunavyowachukulia watu?

Kwa muhtasari: Katika aya hizi, tunaweza kuona dhahiri kwamba Mungu anadhani watu ni wa muhimu sana. Alituumba kwa sura yake — kila mmoja wetu ametengenezwa kwa uangalifu mkubwa katika tumbo la mama yake. Anawajali sana watu hata akamtuma mwanaye afe kwa ajili yatu.

Fikiria tena kuhusu makanisa yaliyokuwa yanawasaidia Malaya huko Congo.

- Je, mawazo haya yanaweza kutusaidia kuelewa kwanini walichagua kuwasaidia hao malaya?

TAFAKARI BINAFSI

Kila mmoja wetu ni wa thamani kwa Mungu. Vivyo hivyo kila mtu katika jamii yako. Chukua muda kutafakari kimya kama unawatendea watu katika jamii yako kana kwamba ni wa thamani sana kwa Mungu.

Mfano wa kujifunzia: Kanisa la Mwanzo

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Wakristo katika kanisa la mwanzo walijua kwamba watu ni wa muhimu. Wakati ule, watu waliamini kwamba miungu walipigana kwa ajili ya ukuu na walitaka watu watoe sadaka kuepuka adhabu za miungu. Wakristo walielewa Mungu wa kweli alikuwa tofauti. Badala ya kutaka sadaka, alijitoa sadaka kwa ajili ya watu, kumtuma mwanaye mpendwa wa pekee afe kwa ajili yao (Yohana 3:16). Kujitoa kwa Yesu Kristo ilithibitisha kwamba kila mwanadamu ni wa muhimu sana na mwenye thamani kubwa. Uelewa huu wa upendo wa Mungu kwa Ulimwengu na wanadamu ulipelekea kanisa la mwanzo kupinga matendo yaliyokuwa ya kawaida wakati huo kama kutoa mimba na kuua vichanga. Kwa wakati ule, kama mtoto wa kike akizaliwa, mara nyingi angetelekezwa mitaan. Lakini, wakristo walielewa kwamba kila maisha— ya ukilema, kabla ya kuzaliwa, wakiume au wakike, mtumwa au mfalme - yalikuwa ya thamani kupita kiasi kwa Mungu. Waliwachukua watoto wachanga mitaani na kuwalea kama watoto wao wenyewe.

Kanisa la mwanzo pia liliamini kwamba kwa kuwa Mungu alionyesha upendo wake kwa kutoa sadaka maisha yake kwa ajili yetu, hivyo iliukwa wajibu wao pia kujitoa kwa ajili ya wengine kisadaka. Wafuasi wa Yesu walielewa kwamba walitakiwa kuwa wenye upendo na huruma kwa watu wote kwa namna ileile Mungu alivyokuwa mwenye huruma na upendo kwao.
Wakati huo huo, mlipuko wa kipundupindu ulitokea. Kama mtu mwenye kipindupindu akinywa maji mengi, nafasi yake ya kuishi ni kubwa. Bila maji, watakufa. Lakini, kipindupindu kinaambukizwa sana. Kwa sababu Warumi waliogopa ugonjwa huu, mara tu walipomwona mtu mwenye huo ugonjwa, walimtupa nje mitaani ajifie huko kuliko kumpa maji. Maisha ya mwanadamu hayakuwa ya muhimu kwao. Wakristo, hatahivyo, walikuwa tofauti. Kwa kweli, walienda kwa wale waliokuwa na kipindupindu na kuwapelekea maji na kuwauguza. Waliamini katika huduma ya kujitoa na huruma. Wakristo wengi walikufa kwa kipindupindu, lakini kama walivyoshuhudia upendo wao, watu wengi walimpa Kristo Maisha yao. Kanisa likakua kwa kasi sana.

TAFAKARI BINAFSI

Chukua muda kuitafakari hadithi hii kimya peke yako
Mwombe Mungu akusaidie kuona jinsi unavyowatendea wengine. Unawatendea kana kwamba Mungu anafikiria ni wa muhimu sana kiasi kwamba yuko tayari kufa kwa ajili yao? Je unawatendea baadhi vizuri na wengine si vizuri sana? Mwombe Mungu msamaha pale ambapo hukuwatendea watu kwa namna inayompendeza. Mwombe akuonyeshe namna anavyowaona watu.

MJADALA KATIKA VIKUNDI VIDOGO

- Ni watu wa aina gani ambao hawathaminiwi kabisa?
- Ni namna gani tunaweza kuonyesha watu kwamba ni wa muhimu kwa Mungu?

Somo la 3: Kumpenda Mungu na kumpenda jirani yetu

Wazo Kuu

Mungu ametuita kumpenda jirani yetu kama njia ya kuonesha upendo wetu kwake. Tunaweza kuonesha upendo kwa jirani yetu kwa kuyafikia mahitaji yao.

Nyenzo

1. Picha za kufundishia:
    a. Igizo la mwinjilisti (nakala 3)

Utangulizi – Igizo la mwinjilisti

Igizo

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Chagua wanakikundi watatu kushiriki katika igizo lifuatalo. Wapatie nakala za picha za vioneshi – Igizo la Mwinjilisti*

Utangulizi wa msimulizi: Wakristo wakati mwingine wana kile tunachokiita "mtazamo finyu wa injili". Wanaelewa kwamba kumkubali Yesu ni uamuzi wa uhai na kifo, lakini hawaelewi kitu kingine zaidi. Wanapokuwa vipofu kwa mahitaji ya jirani, Ujumbe wao kwa kweli unapotea. ... Leo, tutatembelea familia masikini sana. Mkazi pekee, mtu masikini mgonjwa, anaumwa na yuko kitandani. Mgeni, mwinjilisti wa kikristo akiwa katika huduma ya nyumba kwa nyumba, ndio amefika.

Mwinjilisti **MWINJ:** Hodi! Hodi! Kuna mtu yeyote nyumbani? Hodi mpaka ndani! (Anaingia)
Mtu Masikini Mgonjwa (**MMM**)**:** (Kwa unyonge) Niko hapa…
MWINJ: Kwema. Mimi ni _____ kutoka kanisa la _____. Nimekuja leo kumkaribisha kila mtu katika kanisa letu. Mungu ametubariki kwa uamsho wa nguvu sana. Hutataka kuukosa.
MMM: (Akigumia, akiongea kwa kusitasita) siwezi kuja…siwezi kutoka kitandani… naumwa sana hata siwezi kutembea… nimepoteza kazi yangu… sina pesa ka ajili ya dawa… au chakula… au pango la nyumba...
MWINJ: Hayo ni matatizo makubwa sana, lakini namjua mtu mmoja mwenye majibu kwa taabu zote za maisha. Umeishampokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wa Maisha yako?
MMM: (Kinyonge) Ndugu zangu na marafiki walinitelekeza nilipougua na kupoteza kazi yangu… Kuna mtu yeyote kwenye kanisa lako anaweza kunisaidia? Tafadhali? . . .
MWINJ: Msaada bora unaoweza kupata uko hapa katika kipeperushi kidogo cha dini. Kinaeleza Mpango wa Mungu kwa Maisha yako. Unajua, si mpango wake kwamba umelala hapa! Chukua hiki, kisome, Sali sala ya mwenye dhambi, na amini!
MMM: (Mdhaifu zaidi) Siwezi… niko mdhaifu sana… (anaacha kuongea, analala bila kujitikisa.)
MWINJ: (Anasikiliza mapigo ya moyo) Bado yuko hai! Bwana asifiwe, Nimefika kwa muda kushuhudia! Nitaacha kipeperushi. Lazima niende ili nikahudumu kwa roho nyingine zilizopotea. (Akiongea kwa sauti ya juu sikioni mwa MMM) Tutakuombea. Kumbuka, Yesu ni jibu (anaondoka)
MMM:(Anamwangalia akiondoka anagumia) Ohhhhhhhhhhh.....
(Usifanya kitu chochote – au Chochote kinachoonekana kinafaa)

MAJADILIANO YA KIKUNDI KUIKUBWA

- Nini kimetokea katika igizo hili?
- Umeshawahi kuona au kuwafahamu watu wanaotangaza injili namna hii?
- Injili hiyo ilifanikiwa kwa kiasi gani mwishowe?
- Njia hii ya uinjilishaji unailinganishaje na jinsi Yesu alivyohudumu?

Maandiko matakatifu yako wazi jinsi Mungu anavyoguswa na maumivu ya watu—na sisi pia lazima tuwe hivyo. Moja ya "dokezo" bora la kutusaidia kujua moyo wa Mungu kwa watu wake inapatikana katika amri za Yesu.

Amri kuu

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Andika vifungu vya maandiko ubaoni. Waruhusu washiriki waziangalia jozi za aya hizo na wajibu maswali*

Soma aya zifuatazo. Ni mambo gani mawili ambayo tumeamriwa kuyafanya?

Mathayo 22:36-40 Luka 10:27

Soma aya zifuatazo. Aya hizi zinatja moja kati ya mambo mawili yaliyotajwa hapo juu. Ni lipi hilo?

Mathayo 7:12 Warumi 13:9 Wagalatia 5:14

UWASILISHAJI WA TAARIFA

Ni amri zipi mbili katika jozi ya kwanza ya aya tulizozisoma?

- *Mpende Mungu wako*
- *Mpende jirani yako*

Yesu anasema ni ipi iliyo amri kuu kuliko nyingine kati ya hizi amri mbili? (*Soma tena Mat. 22:37-38*)

- *Mpende Mungu*

Enzi za torati (agano la kale) na enzi za unabii (agano jipya) zinaunganishwa na amri moja tu kati amri kuu hizi, ambayo ni ipi?

- *Mpende jirani yako*

Kwa nini unadhani Yesu aliamua kuunganisha Torati na Unabii kwa kutumia amri hii?

- Kama hawatahitimisha kwamba ni kwa sababu tunaonyesha upendo wetu kwa Mungu kwa vitendo, basi rudia swali hili mwishoni mwa somo/kipindi

Kumpenda Jirani yetu

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Soma I Yohana 3:17, I Yohana 5:3, Yakobo 1:27

- Aya hizi zinafundisha nini kuhusu kumpenda jirani yetu?

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Kuna uhusiano gani kati ya Upendo wa Mungu na mwitikio wetu kuhusu mahitaji ya watu?

- Kama tunampenda Mungu, tutaonyesha hilo kwa kumpenda jirani yetu. *Kama tukisema kuwa tunampenda Mungu, lakini hatumpendi jirani yetu, basi inaonyesha kuwa hatumpendi Mungu kwa dhati.*

Je, inawezekana kuelezea upendo wa Mungu bila kusaidia watu kwenye mahitaji yao?

- *Hapana*

Je, sisi tutakuwa wafuasi wa Yesu kama hatuhudumu kwenye mahitaji ya kijamii na kimwili— na pia mahitaji ya kiroho ya mtu?

- *Hapana.Tukiangalia hadithi ya kondoo na mbuzi, tunaona wazi kabisa kwamba tunatengwa kulingana na yale tunayotenda na yale tusiyotenda. "Nalikua na njaa, mkanilisha; nalikua na kiu, mkaninywesha …" (Mathayo 25:35). Yesu anatuambia wazi kabisa katika hadithi hii kwamba anatutegemea tushughulike na mahitaji ya wale waliotuzunguka kama kweli sisi ni wafuasi wake.*

Msalaba

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Chora* picha ya msalaba ubaoni kama inavyoonyeshwa. Elezea picha hiyo kwa washiriki.

Mchoro huu unalenga kutusaidia kukumbuka kanuni hii.

Msitari unaoenda juu unawakilisha uhusiano wetu na Mungu. Ndio msitari mkubwa zaidi.

Msitari uliolalala unawakilisha uhusiano wetu na watu wengine. Msitari uliolala unategemezwa na msitari wa wima. Bila msitari wa wima, msitari wa ulalo ungekuwa kwenye uchafu. Hii ni kweli siyo tu kwa picha hii bali pia kwa Maisha yetu. Tunamhitaji Mungu atusaidie kuwa mahusiano mema.



Jirani yetu ni nani?

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Katika zoezi hili, utasoma hadithi ya Msamaria Mwema wakati watu walioko darasani wakiigiza. Watu saba wanahitajika kusaidia kuelezea kwa vitendo hadithi hii: mtu 1, wanyang'anyi 2, kuhani 1, Mlawi 1, Msamaria 1, mhudumu 1*.

Mtu mmoja alimuuliza Yesu "Nifanye nini ili niweze kuurithi ufalme wa milele?" (akiwa na maana, "Nifanye nini ili niweze kuingia mbinguni") Yesu alimjibu kuwa vitu viwili vilihitajika—kwamba tumpende Mungu na kwamba tumpende jirani yetu. Yule mtu kisha aliuliza "jirani yangu ni nani?"

Yesu alijibu kwa hadithi ifuatayo.
Soma Luka 10:30-37.

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

- Msamaria mwema alimjua mtu aliyelala chini?
- Nini ulikuwa mwitikio wa Msamaria Mwema kwa mtu huyo? Ulitofautianaje na wa watu wengine?
- Msamaria Mwema alionyeshaje upendo kwa jirani yake? Je, alifanya tu cha kutosha au zaidi ya kile cha lazima?
- Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu jirani yetu ni nani?
- Hadithi hii inatufundishaje kuhusu namna ya kuonyesha upendo kwa jirani yetu?

utumikaji

Fikiria watu unaowaona mara kwa mara. Ni kitu gani kimoja unachoweza kumfanyia mtu mwingine?

Somo 4: Kukua katika maeneo yote

Wazo kuu

Yesu alikua katika maeneo manne—kimwili, kiroho, kijamii, na kiakili. Twatakiwa pia kukua katika maeneo haya manne na tuweze kuzisaidia jamii zetu na kanisa kukua vivyo hivyo.

Nyenzo

1. Mwongozo wa mwanafunzi:
    a. Jedwali la ukuaji (moja kwa kila mwanafunzi)
2. Karatasi ndogo zinazoweza kubandikwa kwenye ubao wa matangazo

Utangulizi

MAJADILIANO YA **KIKUNDI KIDOGO**

- Mtoto anahitaji nini ili aweze kukua kati ya umri wa miaka 0 hadi 18

Maelekezo ya mweszeshaji: *Andika majibu yao kwenye vipande vya karatasi (utavitumia vipande hivyo vya karatasi katika zoezi linalofuata). Kama watakosa mifano kutoka kwenye eneo lolote kati ya manne (angalia hapa chini), basi wasaidie kwa kuwapa mfano. Mfano: eneo la kijamii: unadhani mtu huyu angehitaji familia au mtu wa kumpenda?*

Luka 2:52

Soma Luka 2:52: "Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu"

Ni maeneo gani manne ambayo Yesu alikua? Ni maneno gani ya kawaida yanayoelezea namna hizi nne za ukuaji?

- hekima — akili
- kimo — kimwili
- akimpendeza Mungu — kiroho
- akiwapendeza wanadamu — kijamii

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Andika maneno ya kawaida manne kwenye ubao. Chukua kadi. Tumia orodha ya vipande vya karatasi iliyotengenezwa wakati wa utangulizi na waombe washiriki kuvichanganua katika kila eneo.*

Kama Yesu alivyokua, nasi tunahitaji kukua katika maeneo haya manne. Tunaweza kutumia ukuaji wa Yesu kama mfano wa kufikiria namna gani watu wanavyohitaji kukua.

Ukuaji wa Yesu

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

1. Yesu alikulia katika mazingira gani kimwili/ki mali/ kijamii? (Je, alienda chuo kikuu? Alikuwa na umeme nyumbani kwake? Alikuwa na chakula cha kutosha? Aliweza kuandika na kusoma? Alikuwa na wazazi wenye upendo?)
    - *Yesu alikulia katika familia maskini. Walilazimika kutoa sadaka ya njiwa wawili.*

(Angalia Luka 2:24 na Walawi 12:8.)

- *Lakini, alikuwa na chakula cha kutosha. Baba yake alikuwa na kazi, na alikuwa na familia yenye upendo.*
- *Pia alijifunza kusoma na kuandika katika masomo yake kwenye sinagogi.*

2. Je, Yesu alikuwa na rasilimali za lazima kukamilisha mpango wa Mungu kwa ajili yake? Kama ndio kwa nini au kama hapana kwa nini?
   - *Yohana 17:4 inatuambia Yesu alimaliza kazi aliyopewa na Mungu. Aliweza kufanikisha lengo lake.*
3. Ni utajiri kiasi gani unahitajika kufikia mipango ya Mungu
   - *Yesu alikua masikini, laikini aliweza kufikia mipango ya Mungu katika Maisha yake.*
4. Yesu alikua katika maeneo manne. Je, tunaweza kuwasaidia wengine wakue katika maeneo haya? Kwa namana gani?
   - *Ndiyo, haya maeneo manne yanatupatia mfano tunaoweza kuutumia kuwasaidia wengine.*
   - *Kukua katika maeneo haya manne ni mchakato unaochukua muda.*
5. Je, ukuaji wa Yesu ulitokea mara moja au ulikuwa ni mchakato wa hatua kwa hatua?
   - *Ukuaji wa Yesu ulikuwa ni mchakato wa hatua kwa hatua*
6. Kama kuendelea kwa Yesu ulikuwa na mchakato wa miaka mingi, ni kiasi gani cha muda kinahitajika kwa watu wengine kuendelea? Ni muda kiasi gani tunatakiwa tujiandae kuuwekeza katika maendeleo ya watu?
   - *Inachuka muda kwa waatu kuendelea. Kama tunataka kuwasidia kuendelea basi lazima tuwe tayari kuwekeza masaa mengi kwa miaka mingi.*

Utumikaji katika Maisha yetu

Hatuhitaji tu kuendelea katika maeneo manne tu kama Yesu alivyofanya, bali pia kuwasaidia wengine wakue katika maeneo haya manne.

Maelekezo kwamwezeshaji: *Mpe kila mtu nakala ya Jedwali la Luka 2:52: kama huna nakala za jedwali, chora jedwali ubaoni na washiriki wanaweza kulichora kwenye karatasi kwa ajili yao.*

Kwanza, jaza jedwali ukitoa mifano ya namna unavyoweza kukua katika kila moja ya maeneo haya na wahimize familia, kanisa na jamii yako kukua katika maeneo haya.

Kumbuka…

- Chagua mambo yanayweza kufanyika ndani ya wiki moja. Kama ukichagua kitu ambacho ni kikubwa muno, itakuwa vigumu kukikamilisha na matokeo yake yatakuwa ya kuvunja moyo. Chagua kitu kidogo ili uweze kupata mafanikio na unaweza kuchagua kitu kingine wiki ijayo.
- Chagua kitu ambacho haukifanyi kwa sasa.

Makundi ya wasijua kusoma na kuandika*—kama ni vigumu kwa kikundi kujaza jedwali basi jadili maeneo yafuatayo:*

- Fikiria kuhusu namana unavyoweza kukua katika kila moja ya maeneo manne. Ni baadhi ya mambo gani ambayo bado huyafanyi?
- Fikiria kuhusu familia yako. Je, wanakua katika meneo yote manne? Ni kitu gani kimoja unaweza kufanya kusaidia familia yako au mmoja wa wanafamilia yako kukua katika moja ya maeneo haya?

- Fikiria kuhusu kanisa lako – nani unaweza kumsaidia kukua katika moja ya maeneo haya manne? Ungeweza kufanaya nini?
- Fikiria kuhusu jamii yako - nani unaweza kumsaidia kukua katika moja ya maeneo haya manne? Ungeweza kufanya nini?

Jaza sehemu ya jedwalli iliyobaki kwa namna gani unaweza kusaidia familia yako, kanisa lako na jamii yako wakue katika maeneo haya kama Yesu alivyoweza kukua.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Wape wanafunzi muda wa kutosha kutafakari. Ni muhimu kwamba wawe na muda wa kutosha wa kupata mawazo mazuri kuliko kukurupuka na kujaribu kufikiria wazo la kwanza wanaloweza.*

Wakishamaliza, waombe wachache kulishirikisha darasa mawazo yao. Waulize kama kuna sanduku lolote ambalo ni vigumu kupata mifano na uone kama kikundi kinaweza kupata mifano mizuri zaidi kwa pamoja (Kama hakuna muda wa kutosha kwa kila mtu kumaliza, wahimize wanashiriki kuendelea kuifanya kazi hiyo wanapokuwa nyumbani).

Mazingira Kwa ukuaji	**Maeneo ya ukuaji wa Yesu**			
	Hekima	**Kimwili**	**Kiroho**	**Kijamii**
 **Binafsi**	*Soma kitabu au Makala kuhusu eneo ambalo nataka kujifunza zaidi.*	*Tembea mwendo mrefu*	*Chukua nusu siku kufunga kupata muda kukaa katika sala*	*Tuma ujumbe wa kutia moyo kwa Rafiki*
Familia	*kujadili kwa kutumia methali mbili na familia yangu*	*kuosha vyombo baada ya mlo wa familia*	*kuongoza familia yangu katika ibada ya kilasiku*	*Kumtoa mwenza "nje" (Bila watoto)*
Kanisa	*kufanya ibada za Jumatatu kutumia mahubiri ya Jumapili*	*kutengeneza njia ya kutembea mbele ya kanisa*	*kuwaombea kila siku mchungaji na wazee wa kanisa*	*Kukaribisha waamini wa makanisa mengine nyumbani.*
Jamii	*kujadili matatizo ya jamii na kiongozi wa jamii*	*kutembea maeneo jirani kuokota takataka*	*Kukaribisha majirani kusherekea Krismasi nyumbani kwetu*	*kucheza soka na watoto wa majirani.*

HITIMISHO

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO (WATU 2-3)

Katika kikundi cha watu 2-3 (si zaidi ya 3!), kila mmoja awashirikishe wenzake kitu kimoja utakachokifanya. Ombeana ili Mungu awape uwezo wa kukamilisha kile ulichopanga kufanya.

Somo 5: Mungu anataka kanisa lisaidie

Wazo kuu
Wito wa wa kanisa ni kuipenda jamii inayolizunguka kwa vitendo, hasa kwa kugusa mahitaji ya maskini.

Nyenzo
1. Karatasi – vipande viwili kwa kila kikundi chenye watu wane (4)
2. Mwongozo wa mwanafunzi:
    a. Namana ya kusaidia (nakala moja kwa kikundi)

Utangulizi

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO (WATU 4)

Tengeneza orodha ya kazi zote zinazofanywa na kanisa lako (chora picha kuwakilisha kila kazi kama ikilazimu).

***Maelekezo kwa mwezeshaji**: ukishamaliza, waulize vikundi vyote wapitie orodha na waweke alama kama kazi hiyo imeandaliwa kwa watu wanaohudhuria kanisani au kwa wale wasiohudhuria kanisani. Alam ziko ngapi kwa kila moja? Kisha weka alama tofauti kwa kazi zinazolenga masikini na wahitaji. Alama ziko ngapi?*

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA
1. Watu katika jamii wanafikiri nini kuhusu kanisa?
2. Watu katika jamii wanafikiri kanisa hufanya nini?
3. Watu katika jamii wanafikiri nini nkuhusu wakristo?
4. Je, watu katika jamii wanataka kuja kanisani au huwa unalazimika kwenda kuwaalika?
5. Unafikiri watu katika jamii wangejisikiaje kama kanisa lisingekuwepo?
6. Unafikiri hii inamfanya Mungu afurahi?

Isaya 58

Isaya alikuwa anawaandikia Waisraeli, ambao ni watu waliochaguliwa na Mungu. Ni mfano kwa kanisa la leo.

Soma Isaya 58:1-10 na jadili maswali yafuatayo:
- Watu walikuwa wanafanya nini?
- Nini ulikuwa mwitikio wa Mungu kwa watu hawa?
- Kwa nini Mungu alijibu namna hii?

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO (WATU 4-5)
Waombe kila kikundi kifupishe kifungu hiki ama kwa kuchora picha au kuandika sentensi moja.
Baada ya kila kikundi kuwasilisha sentensi au picha yao, waulize wanafikiri mawazo haya yanamaanisha nini kwa kanisa leo.

Chumvi na Mwanga

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO AU KIKUBWA

Soma Mathayo 5:13.

- Matumizi ya chumvi ni nini?
    - *Husafisha, huepusha vitu kuoza, huongeza ladha*
- Kwa nini Yesu anasema wakristo ni "chumvi ya dunia"?
    - *Tunatakiwa kuwa washawishi wazuri katika maeneo tunayoishi. Tunatakiwa kuleta ushawishi wenye utakaso na kuifanya jamii yetu isioze. Hii ina maana kuwa tunatakiwa kuziona jamii zetu zikiwa kama Mungu alivyokusudia, na si vinginevyo.*
    - *Vivyo hivyo, kama ambavyo chumvi kidogo tu hubadili ladha ya chakula, wakristo wachache tu wanaweza kuleta matokeo/mabadiliko makubwa katika jamii*

Soma Mathayo 5:14-16.

- Tunawezaje kung'aa kwa uangavu zaidi?
    - *Kwa kutenda yaliyo mema*
- Ni nini matokeo ya kutenda yaliyo mema?
    - *Baba yetu wa mbinguni anatukuzwa*

Hadithi za chumvi na mwanga

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Soma hadithi 1 – Sari (Mavazi) kwa ajili ya maskini

Wanajumuiya wa kanisa hili walijiona kama kikundi kidogo cha kidini kilicho kandamizwa. Waliogopa kutoa huduma nje ya jamii ya Kikristo. Baada ya kijifunza kuwa wanatakiwa kuudhihirisha upendo wa Kristo kwa jamii nzima, mchungaji aliwahamasisha wanawake wa kanisa kuchunguza mahitaji ya jamii kwa wiki iliyofuata.

Katika ibada ya wiki iliyofuata, wanawake walitoa taarifa kuwa walipata wanawake kumi na wawili wa kihindi ambao kila mmoja wao alikuwa na sari (gauni) moja tu. Wakati wa joto, masari yanatakiwa kufuliwa kila siku. Kama mwanamke ana sari moja tu, hukaa ndani hadi sari lake lililofuliwa likauke. Mchungaji aliuliza kama kulikuwa na wanawake ndani ya kanisa ambaye alikuwa na masari matatu atakayeridhia kutoa moja wapo kwa ajili ya hao wanawake wa kihindi. Wanawake wa kutosha walijitolea sari nyingi hata kuzidi hitaji lililo ripotiwa. Wiki iliyofuata, wanawake wa Kanisa walitembelea kaya ambako wanawake walikuwa na sari moja tu wakawaongezea sari ya pili. Wale wanawake wa Kihindi walivutiwa sana na huduma hii mpaka wakawakaribisha wale wanawake wa Kikristo kuwaombea. Pia baadhi ya wanawake wajawazito wa Kihindi waliwaomba wale wanawake wa Kikristo kuwaombea watoto wao ambao hawajazaliwa.

Soma hadithi 2 –Maji kwa ajili ya Jamii

Katika eneo moja watu walikuwa na upungufu mkubwa wa maji. Baada ya kujifunza hamu ya Mungu kwa Kanisa kuifikia jamii, uongozi wa Kanisa uliamua kuchunguza nini wangeweza kufanya wenyewe kukabiliana na hitaji lao la maji. Walipata mahali ambapo wangeweza kukodi vifaa ambavyo vingeweza kutumika kuchimba visima kwa mikono. Hapo mwanzo, watu walilikataa wazo hilo – walifikiri kuwa maji yalikuwa mbali sana. Kama visima vya kuchimbwa kwa mikono viliwezekana, wakasema, kwa nini hawakuchimba hapo awali? Hata hivyo, uongozi wa Kanisa uliamua kujaribu kuchimba. Wakaazima silinda ya chuma inayoweza kuzamishwa mita kwa mita na "winchi". Wakalileta kwenye jamii yao na kuanza kuchimba maji nyuma ya eneo la Kanisa. Maji yalipopatikana kwenye kina cha urefu wa futi arubaini na tano, kila mmoja alisherehekea kwa shauku kubwa.

Wasio waumini wa Kanisa, hata hivyo, hawakufurahishwa. Walifikiri kuwa waumini wa Kanisa wangetumia maji wao wenyewe tu. Lakini badala yake, Kanisa liliwakaribisha wanajamii kushiriki baraka za Mungu za mafanikio yao ya kisima. Baadaye, wawakilishi kutoka katika jamii za vijiji jirani walianza kuwaomba viongozi wa Kanisa kama wangeweza kuwasaidia kuchimba visima kwenye maeneo mengine yao pia. Kanisa lilikubali. Baada ya mwaka mmoja na siku kidogo hivi, visima kumi na vitano vilichimbwa kwa mkono – kimoja kikiwa na zaidi ya futi themanini.

Watu walivutiwa sana kwa namna kanisa lilivyoonesha upendo wa Mungu kiasi kwamba hata pale Kanisa lilipoikaribisha jamii kuja kusikia ujumbe wa upendo wa Mungu, kanisa lilijaa watu waliokuwa na hamu ya kujua zaidi kuhusu Mungu na watu wake waliowapatia maji.

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

- Makanisa haya yalifanya nini?
- Je, yalikuwa makanisa tajiri?
- Walitumia rasilimali gani?
- Kwa nini walifanya mambo haya?
- Nini yalikuwa matokeo ya matendo yao?

Kondoo na Mbuzi – Mathayo 25: 31-46

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

Maelekezo ya mwezshaji: *Wasaidie wanafunzi waone kuwa msisitizo wa kifungu hiki ni kwa vitu vya kimwili. Yesu hakusema "Nalikuwa na njaa ukanipa kipeperushi" au "nalikuwa hospitali na ukanitumia kanda za mahubiri." Zilikuwa ni suluhu dhahiri kwa mahitaji ya kimwili.*

Somo Mathayo 25:31-46

1. Nini ilikuwa ni tofauti kati ya kondoo na mbuzi?
2. Nini baadhi ya vitu kondoo alifanya? Je ni vya kiroho au kimwili?
3. Mara ngapi kanisa lako hufanya vitu vilivyosemwa na Yesu?
4. Nini yangekuwa ni matokeo kwenye jamii kama waamini wote wa kanisa lako wangefanya vitu hivi?

   Baadhi ya majibu yanayowezekana:
   - *Wangekuwa na taswira nzuri ya kanisa.*
   - *Maisha yao yangeboreka*
   - *Wangekuwa wazi zaidi kujifunza kuhusu Mungu.*

Namna ya kuwasaidia wengine

KAZI YA KIKUNDI KIDOGO

Fikiria namna maalum ambazo kanisa linaweza kusaidia watu katika kila moja ya hali hizi - njaa, kiu, uchi, ukosefu wa makazi, ugonjwa, kifungoni. Tumia jedwali la namna ya kusaidia na mlijaze pamoja jedwali hilo.

Somo 6: Ni mahitaji gani tunaweza kusaidia

Wazo kuu
Mungu anataka sisi tuweze ktatua changamoto zote zinazoikabili jamii yetu. Mungu ana makusudi mema kwa jamii yetu.

Nyenzo

1. Mwongozo wa mwanafunzi:
    a. Mchungaji Wong (nakala moja kwa kila kikundi)
    b. Mfano wa kujifunzia wa Yusufu na Maria (nakala moja kwa kila kikundi)

Maono ya Mchungaji Wong

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO
Maelekezo ya mwezshaji: *elezea darasa kuwa unaenda kuwapa hadithi Fulani. Baada ya kusikiliza, wanatakiwa kusikiliza majibu ya maswali yafuatayo.*

- Ni matatizo gani yaliyopo katika jamii ya mchungaji Wong?
- Nini lilikuwa kusudi la Mungu kwa jamii hii? Pitia kila tatizo na tazama suluhisho alilolitoa Yesu.
- Yesu alimwambia Mchungaji Wong afanye nini?

Soma hadithi ya Mch.wong.

Kulikuwa na mchungaji mmoja wa kanisa dogo katika kitongoji maskini cha jiji kubwa. Jina lake aliitwa Wong. Wong alihamia kwenye hiyo jamii karibuni kwa sababu alihisi ni kama Mungu alimtuma. Kanisa lilikuwa dogo—likiwa na takribani watu 40 hivi. Wengi wao walikuwa wanawake na watoto. Wong alikuwa na kazi mbili. Alifanya kazi kwa bidii kulichunga kundi lake dogo, na alifanya kazi nyingine ili aweze kumtunza mkewe na watoto wake wawili wadogo.

Siku moja, kama ilivyokuwa desturi yake, aliamka saa moja kabla ya kupambazuka ili awe na muda binafsi na Mungu. Aliamka, akavaa, na kupita kimyakimya kwenye pazia lililotenganisha makazi yake ya nyumba yenye chumba kimoja kutoka kwenye eneo ambalo mke wake na watoto waliendelea kulala. Akawasha kibatari chake cha mafuta ya taa. Akaanza kusoma kutoka kwenye Biblia yake. Katika asubuhi hii ya pekee, alikuwa akisoma kutoka Isaya, sura ya 58, na alikuwa akisikia kilio cha Mungu kwa ajili ya aina ya ibada anayotaka:

Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza Kamba za nira, kuwaachia huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Unapomuona mtu aliye uchi, mvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe?

Wong hakuweza kuendelea. Moyo wake ulipigana na akili yake. Kama Mungu aliwajali sana maskini, kwa nini Wong alijikuta mwenyewe katikati ya umaskini na mateso yaliyouvunja moyo wake? Alijua ni namna gani watu wa jamii yake walivyopambana kuishi. Walikandamizwa kweli kweli. Hata yeye hakuwa na chakula cha kutosha kuilisha familia yake na mara nyingi hakuweza hata kuwanunulia dawa walizohitaji. Akafikiri, “Mungu yuko wapi? Maandiko haya yataendana namna gani na mahitaji ya jamii hii?”

Wakati akihangaika na mawazo haya, kulikuwa na hodi mlangoni. “Atakuwa nani huyo, asubuhi na

mapema hivi?" Wong akafikiri. Akaenda mlangoni. "Ni nani?" Sauti ya upande mwingine ikasema, "mimi ni Yesu, Wong." "Nani?" Wong akauliza. Sauti upande wa pili ikajibu "mimi ni Yesu, Wong,". "Nani?" Wong akauliza. Sauti ikajibu, "mimi ni Yesu, Wong". "Wewe ni nani vile, kweli?" Wong akauliza. Sauti ikajibu, "Wong, mimi ni Yesu. Nimekuja kwa sababu nimesikia kilio cha moyo wako. Ninataka unioneshe ni nini kinakusumbua."

Sauti ilisikika kwa uhalisia. Wong kwa umakini akafungua kitasa na kufungua mlango. Ilikuwa bado giza na aliona kivuli, lakini kilionekana kuwa kama alivyomfikiria Yesu kuwa. "Karibu, Bwana" Wong akasema. "Hapana, Wong. Ninataka unitembeze kwenye jamii yako na unionyeshe nini kinausononesha moyo wako." Bado akiwa mwenye mshangao, Wong akakubali, akitahadharisha, "Tutahitaji kutembea kwa umakini—mvua zimekuwa zikinyesha sana, kuna uchafu mwingi, na hatuna vyoo vingi."

Wakiwa wanatembea kwenye mitaa hiyo, Wong alimsimlia Yesu habari za nyumba walizozipita. Ndani ya nyumba ile anaishi mwanamke anayejiuza ilia pate kuwalisha watoto wake. Kwenye kibanda kilichofuata kulikuwa na mume mlevi aliyempiga mkewe na wanawe kila alipolewa—ambayo ilikuwa ni mara kwa mara. Pale ni makazi ya Rais wa jamii hii, fisadi ambaye alipokonya fedha kwa ahadi za kuleta umeme kwa ajili ya jamii —lakini alizila na kuzichezea kamari zote.

Wakapita eneo la wazi katikati ya jamii. Lilikuwa linatakiwa kuwa eneo la mikutano ya kijamii, lakini lilikuwa limejawa na harufu mbaya sana ya takataka na panya wakitambaa. "Unaiona ile nyumba?" Wong aliuliza, akiwa anaonesha kibanda kwenye ukingo wa mlima. "Mwanamke mmoja na watoto wanne wanaishi hapo. Paa linavuja—vibaya mno. Ni maskini sana. Wana kipato kidogo sana cha kuwawezesha kula na kuvaa, na huwa wanaugua mara kwa mara." Kwa wakati huu wawili hawa walikuwa ukingoni mwa mlima ambapo kijiji hiki ilikuwa kimejengwa. Wong akaonesha kwenye umbali kidogo. "Huko chini kabisa—huko ndiko kinamama na watoto hutembea kufuata maji. Hakuna maji kabisa katika eneo hili."

Wong akaanza kukata kona, lakini akasikia kilio. Akatazama kuelekea kwenye hiyo sauti. Ilikuwa ni Yesu—Yesu alikuwa Analia! Wong aliona kuwa vitu vilevile vilivyousononesha moyo wake pia viliusononesha moyo wa Yesu. Wong alianza kuzungumza, lakini Yesu aliunyoosha mkono wake na kuuweka kwa Wong, akamtazama, na kusema, "Wong, nataka nikuonyeshe nini ni malengo yangu kwa ajili ya jamii yako."

Ghafla, Wong alijikuta akiitazama jamii yake. Yesu alianza kuzungumuza, na Wong aliweza kuona mambo ambayo Yesu aliyafafanua—yakitokea! Yesu alizungumzia kuhusu watu wa kanisa la Wong—maskini kama walivyo—wakichangia walichonacho pamoja na majirani maskini zaidi. Kila siku, walitunza mchele kidogo na kuuweka kwenye kopo. Mwisho wa wiki, kila mtu alikuwa na kopo la mchele lililo jaa ambalo walileta kanisani kuchangia, kwa jina la Yesu, na watu wa kwenye jamiii ambao walikuwa na kidogo zaidi yao. Walifanya vivyo hivyo kwa sabuni. Wakinamama wa kanisa waliwatembelea wajane ndani ya jamii na "kuwaasili"—wakiwasaidia kufua, kupika, na kuwatunza watoto walipokuwa wanaumwa.

Yesu alizungumzia kuhusu ajira, na Wong aliona kuwa watu walikuwa na kazi. Si kazi za malipo ya juu, bali kazi zilizoleta heshima na kutoa malipo ya kutosheleza mahitaji muhimu. Yesu alizungumzia kuhusu makazi, na Wong aliona vile vibanda vilivyoingiza baridi na mvua vimebadilishwa kuwa nyumba. Si nyumba za kifahari, bali nyumba zilizokuwa safi na salama. Yesu alizungumzia kuhusu maji, na ghafla kulikuwa na mabomba katika maeneo ya kimkakati ambako kinamama na watoto walikuwa wanapata maji safi. Yesu alizungumzia usafi, na Wong aliona kuwa kulikuwa na vyoo—sio kimoja kwa kila nyumba, bali vya kutosha kwa kila mtu aliyehitaji kutumia. Na jalala la takataka katikati ya jamii ulitoweka. Badala

yake, kulikuwa na miti midogomidogo, na kulikuwa na watoto wakicheka na kucheza, wakipigiana mpira. Yesu pia alizungumzia kuhusu maisha yaliyobadiliswa, na Wong aliona kuwa yule mwanamke aliyekuwa akijiuza mwili wake sasa aliwasaidia watoto wake kwa kazi ya heshima. Yule mlevi sasa alikuwa mume na baba mwenye upendo. Rais hakuwa anatumia fedha kwa udanganyifu, bali alikuwa akiisaidia jamii kweli kweli.

Kisha Yesu akasema, "Wong, litazame kanisa!" Wong akatazama. Lilikuwa limejaa. Kulikuwa na wanaume mle! Watu walikuwa na furaha. Walikuwa wakimsifu Mungu kwa wema wake. Wong alikuwepo, akihubiri, akifundisha, na kuwaongoza watu wake katika Roho na katika matendo ya upendo wa heshima. Yesu akaeleza, "Wong, hili ono ndilo kusudi langu kwa jamii yako. Ninakutaka ushirikishe ono hili na uanze kuwaongoza watu kuelekea huko."

Wong alianza kubisha, "Lakini, Bwana, sisi ni maskini sana!" "Wong," Yesu akauliza taratibu, "ni nani aliyewaongoza wana wa Israeli kuvuka bahari ya Shamu? Ni nani aliyeizidisha mikate na samaki na kuwalisha wanaume elfu tano ukijumlisha wanawake na watoto? Ni nani aliyeyaongeza mafuta na unga wa mjane wa Sarepta ili kuwepo na vyakula vya kutosha kuilisha familia yake kwa miaka mitatu ya njaa? Ni nani aliyeituliza bahari ya Galilaya" "Ni wewe, Bwana," Wong akasema. "Basi, Wong, kuwa mtiifu na ufanye niliyokwambia kufanya. Changia ulichonacho, hata kama ni kidogo. Tangaza nia zangu njema kwa watu wako—vyote vya kiroho na kimwili. Na nitaiponya ardhi yenu!"

Wong alisikia jogoo akiwika. Mke wake alikohoa na kujigeuza upande mwingina wa pazia. Alikuwa amekaa mezani, lakini kibatari kilikuwa kimekwishazimika. Palikuwa pameanza kupambazuka. Wong aliangaza kumtafuta Yesu, lakini hakumuona. Akashangaa, "Hivi niliota ndoto? Yalikuwa maono?" Hakujua, lakini Wong alijuwa alikuwa amekutana na Yesu na kwamba alikuwa na uelewa mpya juu ya mpango wa Mungu kuhusu masikini… na maono mapya ya namna alivyotakiwa kuwaongoza watu wake kuuonyesha upendo wa Mungu ndani ya jamii yake.

MAJADILIANO YA VIKUNDI VIDOGO

Maelekezo mwezeshaji: *Rudia tena maswali yale tokea mwanzo wa somo hili na uwaelekeze wanakikundi kujadili na kushirikisha majibu yao kwa darasa.*

TOA MREJESHO

Umejifunza nini kutoka kwenye hadithi ya Mchungaji Wong na maswali yako ya majadiliano?

- *Mungu ana makusudi mazuri kwa ajili ya jamii yake kimwili na kiroho.*
- *Yesu alimwambia Mchungaji Wong atangaze Malengo yake (ya Yesu) kwa ajili ya jamii.*
- *Kuwa maskini si tatizo kwa Mungu. Tunatakiwa kumtii Yeye.*
- *Mungu ataponya ardhi yetu tunapozifuata njia zake.*

Mfano wa kujifunzia: Yusufu & Maria

KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO

Maelekezo mwezeshaji: *Toa nakala moja ya mfano wa kujifuniza wa Jose na Maria kwa kila kikundi. (kwa kila swali, baadhi ya mifano ya majibu yameorodheshwa kwa maandishi ya kulazwa. Kumbuka haya sio tu ndio majibu sahihi, ila ni baadhi tu ya majibu sahihi)*

Fikiria kwamba jamii ya Jose na Maria inafanana na jamii yako.

Nyumba ya Yusufu na Maria imeungua; hakuna kilichobaki kabisa. Jana, wao - pamoja na watoto wao watano — wali kaa kwa ndugu. Hata hivyo, kuna watu kumi tayari wanaoishi ndani ya hiki kijumba kidogo sana, kwa hiyo hakuna nafasi ya kutosha kwa ajili ya watu saba zaidi. Yusufu ni mkulima, na amekwisha maliza kupanda shamba lake dogo, lakini bado kuna miezi mitatu mbele mpaka atakapovuna. Alitumia hela zote alizokuwa nazo kwa ajili ya mbegu za shamba lake na kila alichomiliki kiliungua na moto.

Je, ni nini mahitaji ya familia hii?

- *Chakula*
- *Makazi*
- *Mavazi*
- *Vyombo vya kupikia*
- *Mahali pa kulala wakati nyumba yao ikijengwa upya.*

Ni vitu gani vilivyopo katika jamii vinavyoweza kusaidia?

- *Watu*
    - *Nguvu kazi kusaidia kujenga nyumba mpya*
    - *Watu wa kusaidia kuandaa chakula kwa wajenzi.*
    - *Watu wa kusaidia kuangalia watoto*
    - *Watu wa kufariji na kusaidia familia*
    - *Watu wa kusaidia kusafisha mahali nyumba ilipoungulia.*
    - *Wafanyakazi wa serikali wanaoweza kutoa msaada wa dharura.*
- *Nyenzo*
    - *Sufuria na vyungu*
    - *Chakula*
    - *Mavazi*
    - *Mashuka mazito*
- *Huduma*
    - *Mahali pa kukaa*

JAMII YETU

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO

Kama unaweza, basi waambie vikundi watembelee kwenye jamii yao kwa dakika10-20 kujikumbusha baadhi ya changamoto za msingi katika jamii yao. Halafu wajibu maswali yafuatayo:

1. Kuna changamoto gani katika jamii yako?
2. Unadhani nini ni makusudi ya Mungu kwa hali hiyo?

KAZI YA KIKUNDI KIKUBWA

***Maelekezo*:** *Kwa kutumia njia ya mbegu za uchaguzi, ainisha changamoto kuu tatu kutoka kwenye changamoto zilizoainishwa na wanakikundi.*

Maelekezo ya kuchagua mbegu:

Mpe kila mtu mbegu kumi kitu chochote kidogo tu chaweza tumika kama mbegu: njiti za meno, majani, mawe, nk.) na waombe waweke mbegu zao katika changamoto zilizopo, wakiweka mbegu

nyingi zaidi kwa miradi wanayodhani ni muhimu. Jumlisha idadi ya mbegu zilizowekwa katika kila changamoto - ile iliyowekewa mbegu nyingi zaidi ni ya muhimu zaidi, ya pili inayofuatia kwa idadi kubwa ya mbegu ni ya pili pia kwa umuhimu na ya tatu kwa idadi ya mbegu ni ya tatu kwa umuhimu.

Mungu anataka kanisa lako lifanye nini?

Chukua changamoto tatu mlizoainisha, na kwa kila moja, ongelea kuhusu kitu mlichonacho katika jamii yenu kinachoweza kusaidia kutatua chagamoto hii. Ongelea kuhusu rasilimali watu, nyenzo, fedha na huduma zilizopo ili kuwezesha kutatua changamoto hizo.

Msali pamoja kuhusu kile mnachokwenda kufanya mkitumia kile mlichojadili.

Somo 7: Hesabu za ufalme

Wazo kuu
Hata walio masikini kabisa wanaweza kutoa.na kadri wanavyotoa, ndivyo watakavyomwona Mungu akizidisha jitihada zao kwa namna ya kipekee sana.

Nyenzo

1. Picha za kufundishia/Vionyeshi:
   a. Jozi ya 1: Isaya 40:29 Ishara (kurasa 5 kwa seti moja tu)
   b. Jozi ya 2: Bahasha za mikate mitano, samaki wawili (bahasha 1 kwa kila kikundi)
   c. Jozi ya 3: Bahasha za eliya & mjane (bahasha 1 kwa kila kikundi)
   d. Jozi ya 4: Bahasha za mjane na sarafu zake mbili (bahasha1 kwa kila kikundi)
   e. Jozi ya 5: Bahasha za hadithi ya talanta (bahasha 1 kwa kila kikundi)

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Katika somo hili, utahadithia habari tano katika kitabu cha biblia na uwaambie wanafunzi watengeneze "njia za kihesabu" kutoka kwenye kila hadithi kwa kutumia vioneshi. Kama kikundi hakielewi vizuri hesabu, basi tumia kadi zinazoeleza walichokuwa nacho kabla na baada. Waombe washiriki wachambue picha katika mafungu mawili – kabla na baada. Waulize, "Kuna tofauti gani kati ya mafungu haya mawili? Watu waliendaje kutoka fungu namba moja hadi namba mbili?". Jibu ni MUNGU. Hakikisha wanaelewa kwamba Mungu ndiye aliyesababisha uzidishaji huu.*

Utangulizi: Isaya 40:29

Umeisha ona kwamba Biblia ina kanuni za hisabati ndani yake? Katika somo hili, tunakwenda kuona baadhi ya hesabu zilizoko kwenye biblia.

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA.
Soma Isaya 40:29. Eleza kwamba hii itakuwa aya ya msingi kwa somo hili.

- Nani ni mwenye nguvu? Nani ni mnyonge?
- Mungu anatufanyia nini?
- Je, tunaweza kuweka aya hii katika njia za kihesabu? Ngoja tujaribu...

Maelekezo kwa mwezeshaji: Kama una kikundi kikubwa, Waite watu watano mbele na uwape kila mmoja maneno au alama za hisabati (Vioneshi: jozi ya kadi ya 1). Kwa kikundi kidogo, weka kadi sakafuni na mfanye kazi pamoja kuziweka katika mpangilio sahihi.

"Udhaifu wetu x Mungu = Nguvu"

Tunaweza kujifunza nini katika aya hii — "kanuni" hii?

- *Ni Mungu anayezidisha*
- *Nguvu ya Mungu ni muhimu sana, wala sio udhaifu wetu.*

“Mvulana na chakula chake”: Yohana 6:1-14

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Kwa kila hadithi katika somo hili, jiandae kusimulia hadithi kwa ubunifu.*

Kulikuwa na mtoto mdogo. Alisikia kwamba mwalimu maarufu alikuwa anakuja katika bahari Galilaya na alitaka kwenda kumsikia akiongea. Alimwomba mama yake, lakini alikataa. Ilikuwa mbali sana na chakula cha mchana kilikuwa karibu kiko tayari. Alimwomba tena na tena na mwishowe mama yake alikubali. Alimfungia chakula kidogo katika kitambaa chake na akaanza safari.

Hatimaye alipofika mwisho wa safari, aligundua tayari watu walikuwa wamejaa. Kama mtoto yeyote, alijipenyeza kwenye makutano hadi mbele kabisa. Mwishowe, alipata sehemu ambako angeweza kwa urahisi kumsikia mwalimu na wafuasi wake. Hakuweza kuamini jinsi mwalimu alivyokuwa akiongea na mambo aliyokuwa anasema. Alisahau kabisa kwamba alikuwa bado hajala chakula chake.

Hatimaye, maumivu ya njaa yalipozidi sana akakumbuka chakula ambacho mama yake alikuwa amemfungia. Polepole alifungua mfuko wake akiendelea kumsikiliza mwalimu.

Ghafla, mwalimu aliacha kufundisha na kuwaambia wanafunzi wake wawape chakula kila mmoja. Mvulana aliangalia na kuona makutano yameongezeka hadi watu wanaume 5,000 lakini pia wanawake na watoto. “Wow!” alishangaa,” watawezaji kutengeza chakula kwa watu wengi hivi?” Alipokuwa akishangaa, wanafunzi nao walionekana kuwa na mashaka ya namna hiyo na mmoja wao alimuuliza mwalimu wapi wangepata hela ya kununua chakula cha kulisha makutano makubwa hivyo. Ingechukua angalau nusu ya mishahara ya mwaka mzima ili waweze kupata mlo mmoja.

Mwalimu akawauliza, “Je mna nini?” Mvulana alianza kuficha chakula chake, lakini alikuwa kachelewa. Msaidizi mmoja, Andrea, alimwona. “Mwalimu,” akasema, “Huyu kijana ana vipande 1,2,3,4,5 vya mkate na samaki 2.” Mwalimu akajibu, “Vilete kwangu.”

Unaweza kufikiri kilichotokea baada ya hapo?

Andrea akamwambia mtoto, “Mwalimu anataka chakula chako.” Mtoto akakubali kumpa Andrea chakula, ambaye naye alimpa mwalimu.

Mwalimu alichukua chakula cha mvulana akashukuru, kisha wakaanza kugawa chakula. Mvulana alitoa macho kwa mshangao akiona wasaidizi wakiendelea kuwadumia watu chakula. Kila mtu alikula na kuendelea kula hadi akashiba. Aliangalia na akaona kulikuwa na vikapu 12 vya makombo.

Sasa alikuwa na shauku sana afike nyumbani amsimulie mama yake. Alikimbia njia nzima wakati akirudi nyumbani na akamsimulia mama yake kwamba chakula chake kimelisha watu 5,000 wanaume, wanawake, na watoto! Mama yake alipumua, “Mwanangu, ni mara ngapi nimekukataza kujitungia hadithi za uongo!”

- Tunawezaje kubadilisha hadithi hii kuwa kanuni ya kihesabu?

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO (WATU 3-4)

Maelekezo kwa mwezeshaji: Wape kila kikundi bahasha yenye vikaratasi vya “mvulana na chakula chake cha mchana” (jozi ya 2 ya kadi za vioneshi) au tengeneza alama kubwa na uombe washiriki watengeneze kanuni pamoja. Wape mapendekezo kuwasaidia kupata majibu. Kikundi kikiishafanya

kanuni moja ya hesabu pamoja, wanaweza kufanya yote yaliyobaki katika vikundi vidogo.

Jibu: "mvulana + mikate 5 + samaki 2 x Yesu = chakula kwa 5000 + wanawake na watoto + vikapu 12"

sasa hiyo ndiyo hesabu ya ufalme!

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

- Je, Yesu alimhitaji mvulana na chakula chake? Je, kulikuwa na namna nyingine ambayo angeweza kulisha watu?
- Kwa nini Yesu alichagua kuchukua chakula pekee cha mtoto?

Wakati tukiendelea kutafakari maswali haya, tutaendelea kufanya hesabu za Ufalme zaidi.

"Mjane na chakula chake cha mwisho": 1 Wafalme 17:7-16, 18:1

Ulikuwa ni wakati mgumu sana kwa historia ya Israeli. Nchi ilikuwa na njaa kali kwa miaka mitatu na nusu. Watu walikuwa wanakufa. Hata Eliya, nabii wa Mungu, aliteseka.

Lakini Mungu alimtumia mjane kumtunza Eliya. Eliya alipokuwa akitembea mjini, alimwona mwanamke akiokota kuni na Mungu alimwambia kwenda kwake na kuomba "maji ya kunywa kidogo kwenye chombo." Mwanamke alikubali kumpa Eliya maji, lakini kabla hajafanya hivyo, Eliya kisha alimwomba kama anaweza pia kumletea mkate ale kwanza, hata kabla yeye na mtoto wake hawajala.

Mwanamke akajibu, "Kama Bwana aishivyo, nina chakula cha kutosha kwa mlo mmoja tu, kwa mtoto wangu na mimi, na kisha tutakufa hakika!" Kwa hili Eliya alimjibu, "Usiogope, Bwana atatoa."

Mwanamke aligeuka akaenda na kutengeneza chakula kwa ajili ya Eliya kutoka kwenye kiasi cha mafuta na unga alivyokuwa navyo. Bado alipokuwa ametumia mafuta yake yote na unga kuandaa mkate kwa ajili ya Eliya, alishangaa kuona madumu yake ya mafuta na unga yamejaa tena, kana kwamba hayajaguswa. Mwanamke akamwambia Eliya, "Nilitumia vyote nilivyokuwa navyo kwa ajili yako, lakini sasa kila kitu kimerudi. Bwana asifiwe!"

Biblia inatuambia siyo tu Mungu alitoa chakula cha kutosha kwa ajili ya Eliya, na familia mwanamke mjane siku hiyo, lakini pia alitoa chakula cha kutosha kwa mwanamke na familia yake kula kwa miaka mingine mitatu! Muujiza.

- Tunawezaje kubadilisha hadithi hii kuwa kanuni?

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO

***Maelekezo kwa mwezeshaji*:** *Gawa bahasha (jozi ya 3 ya kadi za vionyeshi) na uruhusu kila kikundi kijaribu kutengeneza kanuni.*

Katika bahasha ya wananojua kusoma na kuandika kidogo, Weka maneno au alalama kwa:

- *mjane*
- *keki 1*
- *Chakula kwa watu 3 kwa miaka 3*

Jibu: " mjane + keki 1 x Mungu = keki1 x watu 3 x siku 365 x miaka 3 = 3,285"

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

- Je, mwanamke alikuwa maskini?
- Je, Mungu angeweza kumlisha Eliya kwa namna nyingine?
- Kwa nini Mungu alimwambia Eliya aende kwa mwanamke mjane tena masikini na aombe kupewa chakula?
- Kwa nini Mungu alimwomba mtoto chakula chake cha pekee katika hadithi ya mikate na samaki?
- Je, Mungu ana moyo kwa masikini na wajane?

"Mjane na sarafu zake mbili": Marko 12:41-44

Siku moja Yesu alipokuwa kwenye hekalu akikaa karibu na kikapu cha matoleo, aliona matajiri wakijionyesha walipokuwa wakitoa sadaka. Mwanamke mmoja maskini alikuwa na sarafu mbili. Kwa sababu ilikuwa ni hizo tu alizokuwa nazo, aliona haya (aibu) na hakutaka watu wengine waone, alitoa sadaka yake kimyakimya, kwa siri. Yesu aliwakusanya wanafunzi wake na akawaambia, "Mwanamke huyu ametoa zaidi kuliko wengine wote."

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

- Yesu alimaanisha nini? Alitoaje zaidi?
- Kwa nini hakumwambia "Hapana, mama, unauhitaji zaidi ya hekalu." Angeweza, lakini hakufanya hivyo. Kwa nini?

Badala kumsimamisha, Yesu aliangalia sadaka yake kwa jicho la pekee. Tangu wakati huo, hadithi ya utoaji wake imeandikwa kwa wengi ili waisome. Wakati ni kweli alitoa zaidi kwa kulinganisha, ila ni kweli alitoa zaidi ya wengine. Kwa zaidi ya miaka 2,000, wakristo wamehamasishwa naye. Fikiria kiasi gani kimetolewa kutokana na mfano wake. Huku ndiko kuzidisha KUKUBWA ZAIDI. Alitoa alichokuwa nacho na Mungu alikizidisha. Hiyo ndiyo hesabu ya ufalme!

KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO

Tumia kadi ndogo ili kujaribu kutengeneza kanuni za hisabati.

Jibu: "mjane + sarafu 2 x Mungu = zaidi ya miaka 2,000 ya ushawishi!"

Likumbushe darasa kuwa:

- Mungu alimwomba mtoto ampe chakula chake cha pekee…
- Alimwomba mjane alimlishe Eliya kwanza, akimpa chakula chake cha mwisho…
- Alimruhusu mjane huyu kutoa chote alichokuwa nacho…

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

- Je Yesu alimsamehe maskini asitoe sadaka?
- Kuna chochote ambacho ni "kidogo sana" au "si cha muhimu sana" kutoa kwa Mungu?
- Je, Mungu hubariki utoaji wa maskini?
- Ni kwa namna zipi Mungu hubariki utoaji wetu?"

- *Baraka za vitu*
- *Kuona Maisha ya wengine yakibadilishwa*
- *Mabadiliko katika jamii*
- *Kuokolewa kwa maisha*

Wakati tunapokuwa tunahisi kupata baraka ya vitu, huwa sio hivyo wakati wote. Wakati mwingine Mungu hutubariki kwa kutufanya kuwa sehemu ya kuleta madiliko katika jamii zetu au kuona watu wengine wakimpokea Kristo. Japokuwa wakati mwingine hutubariki kwa vitu. Tunakumbushwa katika 1 Wakorintho 9:11 kwamba sababu ya Mungu hutubariki ni ili tuendelee kuwa wakarimu katika kila tukio ili Mungu atukuzwe.

Hadithi moja ya mwisho. Huyu hapa hana furaha sana…

"Fumbo la talanta": Mathayo 25:14-30

Kulikuwa na Tajiri mmoja aliyeenda safari ya mbali. Kabla hajaondoka, aliwaita watumishi wake watatu. Wa kwanza, alimpa talanta tano (talanta ni kiasi kikubwa cha fedha) na akasema, "ifanyie kazi hadi nitakaporudi." Wa pili, alimpa talanta 2 na akasema, "Ifanyie kazi hadi nitakaporudi." Na mwisho, wa watatu, alimpa talanta moja na akarudia "Ifanyie kazi hadi nitakaporudi."

Yule Tajiri aliondoka na baada ya muda mrefu alirudi. Kwa mara nyingine tena aliwaita watumishi wake watatu akawauliza walichofanya wakati hayupo. Wa kwanza alimtaarifa kwamba alitumia talanta za bwana wake na alikuwa amezalisha talanta tano zaidi. Kwa huyu Tajiri yule akajibu akasema, "Kazi nzuri! Umekuwa mwaminifu kwa vichache, sasa pata vingi zaidi" Mtumishi wa pili naye alitoa taarifa alikuwa amepata talanta mbili zaidi na kwa huyu pia yule Tajiri akasema, "Kazi njema! Umekuwa mwaminifu kwa vichache, sasa pokea zaidi."

Kisha mwishowe, mtumishi wa tatu akaeleza, "Najua wewe ni mtu mgumu na katili. Niliogopa kupoteza talanta uliyonipa kwa hiyo niliificha. Haijapotea." Kwa huyu yule Tajiri akajibu, "mtumishi mzembe na mwovu!" Akachukua talanta yake, na kumpa mtumishi wa kwanza, na akamtupa nje ya ufalme.

Hii pia, ni hesabu ya ufalme. Ebu tuone

KAZI YA KIKUNDI KIDOGO

***Maelekezo kwa mwezeshaji*:** Gawa bahasha (jozi ya kadi namba 5 ya vionyeshi) na ruhusu kila kikundi kijaribu kutengeneza kanuni.

Jibu: "mtumishi + talanta 1 x 0 (kutofanya chochote) = 0 nyongeza + mtumishi aliyetupwa gizani"

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

- Nani aliyepewa kiasi kidogo zaidi? Lakini ona kilichotokea!
- Je, Mungu hawajali maskini? Kwa hiyo kwa nini alitupwa nje ya ufalme?
- Kuna matokeo gani, hata kwa masikini, wasipomtii Yesu?

Hitimisho

1. Tumekuwa wakarimu kwa kile ambacho Mungu ametupatia?
2. Je, kanisa letu limekuwa na ukarimu kwa kile Mungu ametupatia, au tumekitumia kwa maslai yet utu?
3. Ni kwa namna gani tumeona Mungu akitubariki kwa vile tumekuwa wakarimu?
4. Ni mabadiliko gani ninaweza kufanya ili kutumia kanuni hizi katika Maisha yangu na kanisa langu?

Somo la 8: Vitendo vya upendo

Wazo kuu

Tunaweza kuipenda jamii yetu kwa kuonesha vitendo vya upendo. Tabia za kitendo cha upendo (tendo jema) ni: kinafanywa kuonesha upendo wa Mungu, kinafanywa kwa ajili ya kumtii Mungu, kinafanywa kwa nguvu za Mungu, kinafanywa ili Mungu atukuzwe, kinafanywa kwa kutumia rasilimali zinazotuzunguka, kidogo na kirahisi kufanyika.

Nyenzo

1. Tuzo ndogo kwa shughuli ya rasilimali zinatuzunguka

Utangulizi

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

- Ni mambo gani ambayo kwa kawaida huwa mnayafanya kama kanisa kuonesha upendo kwa wale wasio wakristo katika jamii yako?
- Watu wangapi hushiriki?
- Ni mara ngapi mnafanya vitu/mambo hayo?
- Huwa mnaamuaje nini cha kufanya?
- Mwitikio wa watu ukoje?
- Kwa nini mnafanya mambo hayo?

Vitendo vya upendo

Katika masomo machache yaliyopita tumekumbushwa ni kwa kiasi gani Mungu anampenda kila mmoja. Tumeona pia kuwa tumeamriwa kuwapenda jirani zetu. Vitendo vya upendo ni moja kati ya njia hizo tunazoweza kuzifanya kuonesha upendo huo.

Vitendo vya upendo ni miradi midogo inayofanywa na kanisa kuonesha upendo wa Mungu kwa jamii. Kwa kawaida ni vitu virahisi na vinaweza kufanyika kwa siku moja.

Kuna tabia saba maalumu za tendo la upendo. Katika somo hili tutazipitia tabia hizi saba.

1. kinafanywa kuonyesha upendo wa Mungu

Moja ya malengo ya kitendo cha upendo ni kuonyesha upendo wa Mungu kwa jamii yako.

Katika jamii moja, kanisa liliamua kufanya kitendo cha upendo. Walijisikia kwamba Mungu aliwaambia wakamsaidie mke wa kiongozi wa majambazi katika eneo hilo. Walikuwa wanaogopa sana, maana huyo kiongozi wa majambazi alikuwa na tabia za kuchukia na kuwapiga watu hata kwa sababu ndogo ndogo. Hata hivyo, kanisa lilitaka kumtii Mungu. Walisubiri mpaka pale walipojua kuwa jambazi huyu alitoka nje ya mji wao, halafu wakaenda kmsaidia mkwe wake kuvuna mazao na kuyaandaa tayari kwa kuyauza. Jambazi huyu aliporudi nyumbani, aliona mazao yote yamevunwa na akaanza kupiga kelele. “Nani kafanya hivi?” Mke wake aliogopa kumwambia, akiogopa kuwa ataleta vurugu lakini mwishowe akakiri kuwa ni kanisa ndilo lililomsaidia. Kiongozi huyu wa majambazi akaelekea kanisani na kugonga mlango. Baada ya kuwaita wazee wa kanisa kwa msaada, mchungaji

alifungua mlango na jambazi akaingia ndani. “Kwa nini mmefanya hivi?” aliuliza. Walimjibu kirahisi tu kwamba walitaka kuonesha upendo wa Mungu. Akaanza kulia, akishuhudia ya kwamba hakuna mtu hata mmoja aliyewahi kumpenda katika maisha yake yote. Alibadilika na kuwa mkristo, akaachana na Maisha yake ya kijambazi, na akawabadili familia nyingine sita kuachana na ujambazi na kuwa wakristo.

- Ni nini matokeo ya tendo hili la upendo?
- Je, unadhani kiongozi huyu wa majambazi angekuwa na mwitikio huo huo kama wangeenda kumhubiria injili tu?

Lengo kuu la kitendo cha upendo ni kutii amri ya Mungu kwa kuwapenda jirani zetu. Tunataka kuonesha upendo wa Mungu kwa jamii zetu. Kwa kuanzia, ni vizuri kufikiri kuhusu wale ambao hatukuwaonesha upendo mara kwa mara, kwa mfano wale wasiohudhuria kanisani

- Je, kw nini unadhani ni muhimu kuonesha upendo wa Mungu kwa wasio wakrito?
    - *Wasio wakristo wengi hawapo tayari kuja kanisani kusikia habari za Mungu. Hata hivyo, kama tulivyoona katika hadithi iliyopita, wanapoona upendo wa Mungu, inaweza kuwa na matokeo mazuri sana*

2. Kinafanywa kwa kumtii Mungu

Katika yote, tunatakiwa kuhakikisha tunatembea daima katika utii kwa Mungu. Badala ya kufanya utafiti wa kujua mahitaji ya jamii na kuweka mpango wetu wa kusaidia kutokana na utafiti, tunatakiwa tuanze na maombi, tumwombe Mungu atuambie tufanye nini. **Mara nyingi vitendo vya upendo vyenye matokea makubwa si vitu vya maana sana.**

Fikiri juu ya hadithi tuliyoisoma ya kiongozi wa majambazi

- Kanisa lilifikiaje uamuzi wa nani wamwoneshe Upendo wa Mungu?
    - Waliomba na Mungu aliwaonesha kuwa wanatakiwa kumpenda kiongozi wa majambazi
- Je, unadhani wangeweza kutilia mkazo wa kumfikia kiongozi wa majambazi tu kama wangefanya utafiti wa kijamii wa mahitaji?

Wakati mwingine mambo ambayo Mungu anatutaka tuyafanye hayaleti maana katika namna yetu ya kufikiria – kama kumpenda kiongozi wa majambazi. Lakini, tunaweza kuwa na uhakika kwamba kama Mungu anatuongoza kufanya kitu, kitakamilika hasa kile anachotamani na tutabarikiwa kwa kushiriki katika mpango wake.

3. Vidogo na Rahisi

Unapoanza kufanya vitendo vya upendo, tunakuhimiza kuchagua vitu ambavyo ni rahisi sana. Ikiwezekana, ambavyo vinaweza kufanyika kwa siku moja.

- Kwanini unafikiri ni muhimu kuanza na vitendo vidogo na rahisi vya upendo?

Fikiri juu ya mambo haya manne: tunapoanza na vitu vidogo na virahisi…

1. **Tunaweza kuvikamilisha.** Ikiwa tutafanya kitu kikubwa basi ni rahisi kuzidiwa na ikawa vigumu kukamilisha. Lakini, ikiwa tutafanya kitu kidogo na rahisi itakuwa rahisi kukifanya na kukikamilisha.
2. **Watu wengi zaidi wanaweza kushirikishwa.** Ni rahisi kwa watu kujitoa kwa mradi mdogo kama wanajua ni kwa siku moja au mchana mmoja tu. Watasema “ah, Naweza kufanya hicho kitu.

Nina muda mchana huo". Lakini kwa mradi mkubwa (unaochukua siku nyingi kukamilika) watu wanasita sita zaidi kujitoa kwa muda na rasilimali zao. Hii nikweli hasa kama wazo la kufanya kitu kwa ajili ya mtu mwingine bado ni jipya kwao.

3. **Tunapata fursa kujenga ujuzi wetu.** Labda hatukuwa na uzoefu mkubwa wa kufanya miradi. Hii inatupa fursa ya kufanya kitu kirahisi na kupata uzoefu kabla hatujajaribu kufanya kitu ambacho ni kigumu zaidi
4. **Tunapata mafanikio kwa haraka.** Tunapopata mafanikio katika miradi midogo, watu wengine hasa wanaovutiwa na mafanikio watatuunga mkono. Mwanzoni mnapoanza, watu wachache kanisani watavutika kushiriki. Lakini kadri unavyofundisha watu zaidi na wanapoona miradi inayofanikiwa watu wengi zaidi watatamani kujiunga.

Ni bora kufanya vitendo vidogo vya upendo mara nyingi (mara moja kila wiki au wiki mbili) kuliko mradi mkubwa usioisha. Aidha pamoja na faida zote za kufanya vitendo vya upendo kama vilionyeshwa hapo juu, kuvifanya kila mara pia husaidia kutoa picha ya kanisa linalojali katika mitazamo ya watu kwenye jamii.

4. Vinafanywa kwa kutumia rasilimali zilizopo

ZOEZI LA WENZA

Tutakwenda kucheza mchezo. Fikiri juu ya vitendo vya upendo vinavyoweza kufanywa na kanisa lako kwa watu bila kutumia fedha hata kidogo. Orodhesha kwa kadri uwezavyo. Wenza wenye majibu mengi ndani ya dakika tano watapata zawadi

Maelekezo kwa mwezeshaji: *baada ya dakika mbili, wakumbushe kufikiria kuhusu ujuzi wote ambao watu wanao katika kanisa lao ambao ungeweza kutolewa. Baada ya dakika tano, waruhusu wenza kushirikishana ni vitendo vingapi vya upendo wamevifikiria. Toa zaidi ndogo, kwa mfano chakula wakipendacho, kwa wenza watakaokuwa wameorodhesha vitendo vingi zaidi.*

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA

- Kwa nini unafikiri ni muhimu kufanya kitendo cha upendo kwa kutumia rasilimali zilizopo katika jamii yako?
    - **Ni zaidi ya kuuelezea upendo**
      Kumbuka juu ya hadithi ya sari katika somo la 5. Je, unadhani ingeweza kuwa na matokeo sawa kama shirika kubwa lisilo la kiserikali lingeleta hizo sari katika jamii ile? Hapana, isingewezekana.
        - Kwa nini watu walijisikia kupendwa?
          Ni kwa sababu waliona upendo wa kanisa kwa walivyojitolea. Kama jamii haitaona sadaka ya kujitoa au jitihada zikifanyika kwa bidii, hawataweza kuona upendo wa Mungu kwao kwa njia hiyo.

    - **Baraka ya utoaji.** Soma 2 Wakorintho 9:6-11. Mungu ametuambia kwamba atatubariki kwa kipimo kile kile tunachotoa. Hata hivyo, angalia tena katika aya hizi.
        - Kwa nini Mungu anatubariki
          1. Ili tuweze kuwa wakarimu kwa kila tukio
          2. Ili Mungu aweze kutukuzwa

    Kwa kadiri makanisa yalivyotoa kwa ukarimu, tumeyaona yakibarikiwa na Mungu. Yameanza kuondokana na umasikini. Lakini la muhimu zaidi, yameweza kuwa na ukarimu zaidi n ahata kufanya matendo ya upendo zaidi.

5. Kufanywa kupitia nguvu ya Mungu

Soma Yohana 15: 1-8.

- Kifungu hiki kinatuambiaje kuhusu kiasi gani tunaweza kufanya sisi wenyewe? Unadhani hii inamaanisha nini?
- Tunawezaje kuzaa matunda mengi?

Kusaidia watu kunaweza kuwa kugumu sana. Mungu pekee ndiye anayeweza kuleta mabadiliko tunayokusudia kuona katika jamii yetu. Kama tunataka jamii zetu zikibadilika kupitia vitendo vya upendo, tunahitaji kumtafuta Mungu na kumwomba atusaidie.

Daima tufanye maombi kabla ya, wakati wa, na baada ya kufanya vitendo vya upendo. Tunapokutana na changamoto au vikwazo, tumwombe Mungu atengeneze njia mpya ya kupita. Kama tukichoka au kukata tamaa, hatuna budi kumwamini Mungu atutie nguvu za kusonga mbele.

6. Washirikishe watu wengi kadri iwezekanavyo

KAZI YA KIKUNDI KIKUBWA

Maelekezo kwa mwezeshaji: *ligawa kundi katika vikundi vidogo – A na B. Waombe kikundi A wachague mtu mmoja wa kuwawakilisha. Waambie kikundi cha pili kuwa wote watashiriki. Elezea katika makundi yote mawili kwamba wanatakiwa waunganishe pande mbili za chumba hiki kwa kutumia kitu chochote wanachoweza kupata. Kwenye kundi la A, yule mtu mmoja lazima afanye kazi yote, lakini wanaweza kuazima vitu kutoka kwa wengine. Katika kikundi B, wanaweza kufanya kazi pamoja na kuweka vitu ili kuunganisha pande mbili za chumba. Waeleze kikundi A kuwa hakuna atakayeruhusiwa kuzungumza wakati wote wa zoezi hili. (Kama wakizungumza, waambie "tafadhali nyamazeni, timu ya huduma ipo kazini")*

Makundi yote yanapokuwa yamemaliza kazi, waulize:

- Nani alimaliza wa kwanza?
- Unadhani, ni kipi tunaweza kujifunza katika zoezi hili?
- Kundi A
  - Aliyefanya kazi peke yake amejisikiaje?
  - Na nyie mliobaki bila kufanya kazi, mmejisikiaje? Je, mlitamani kushirikishwa?
- Kundi B
  - Je, mnadhani ni nini faidi ya kuwa na watu wengi wakifanya kazi pamoja?
- Tunapofanya vitendo vya upendo, tunajitahidi kuwashirikisha watu wengi kadri iwezekanavyo – kwa nini unafikiri hiyo ni muhimu?

Mara nyingi, kanisani, watu wachache hufanya kazi zote. Watu hao wanaweza kuchoka mapema san ana hata kukata tamaa, wakati watu wengine wanaweza kuishia kujisikia vibaya tu au ni kama karama/vipawa vyao havitumiki ipasavyo. Hawakui katika ujuzi wao lakini pia hata Imani zao. Wakati mwngine huwa tunakasirika tunapoombwa fedha bila hata kushirikishwa. Unapofanya kitendo cha upendo (tendo jema), unatakiwa kuwashirikisha watu wengi kwa kadri iwezekanavyo kutoka kanisani kwa kile ukifanyacho. Kwa kufanya hiyo, tunafaidika na ubunifu na nguvu ya watu wote. Kitendo kizuri cha upendo sio tu kukusanya kutoka kwa kila mmoja na kutoa, lakini pia kuwashirikisha kila mmoja wao katika kuufanya mradi ho pamoja. Baadhi ya miradhi ambayo makanisa mengine yaliamua kuchagua kuwashirkisha kila mtu ni pamoja na: kusafisha mfumo wa maji, kufagia uchafu kutoka kwenye mitaro ya maji au barabarani, na kufanya usafi kwenye zahanati

7. Kifanyike ili Mungu atukuzwe

Soma Yohana 15:8.

- Nini kusudi la kuzaa matunda mengi?

Soma Mathayo 5:13-16

- Kwa nini tunatenda matendo mema?
- Shabaha yetu iwe nini tunapotenda matendo ya upendo?

Tukishafanya kila kitendo cha upendo, tuchukue muda kutathmini. Nini yalikuwa matokeo ya mradi huu? Fikiria kuhusu maeneo haya matatu:

1. Je, watu walisaidiwa?
2. Je, mradi ulifanyika kwa upendo?
3. Je, Mungu alisifiwa?

Wakati mwingine, watu wanaweza kuguswa na matendo yetu ya upendo na kufunguka kwa ajili ya kusiliza habari za Mungu. Lakini si mara zote. Ukweli ni kwamba sio kila mara tunapofanya kitendo cha upendo tunapata fursa ya kumwongelea Mungu. Lakini wakati wote tunaweza kumtukuza Mungu kwa kufanya vitu kwa namna ambayo inampa heshima. Hata mtazamo wetu, furaha yetu na malengo yetu kuwatumikia wengine yanaweza kuwa ni ushuhuda unaomletea Mungu sifa na heshima.

Hitimisho

Maelekezo kwa mwezeshaji: Eleza kuwa katika soo linalofuata, tutaenda kupanga kitendo cha upendo. Kama unafundisha kila baada ya wiki moja, tenga muda wa kufikiria wiki hii kanisa lako litafanya nini kama kitendo cha upendo.

Hitimisha kwa kurejea kazi za kufanya mara kadhaa zaidi

Somo 9: Kupanga matendo ya upendo

Wazo kuu

Lengo kuu la somo hili ni kupata muda wa kuandaa kitendo cha upendo.

Nyenzo

1. Karatasi kubwa kwa watu 5 - 7

Hatua za kupanga

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO (WATU 5-7)

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Kama unafundisha kanisa la mtaa (local church) ni rahisi kufanya hivi kwa pamoja. Waongoze katika hatua za kupanga vitendo vya upendo.*

Hatua 1: Maombi

Kitu cha kwanza cha kufanya ni kuomba. Chukua muda sasa wa kuomba. Mwombe Mungu akuonyeshe nini ufanye kwa ajili ya tendo la upendo. Hakikisha unapata muda kidogo wa ukimya ili kumsikiliza Mungu.

Hatua 2: Kuchagua shughuli

Kama kikundi, muamue kitu gani cha kufanya kama kitendo cha upendo. Je, mnahisi Mungu anawaongoza mfanye? Kama kuna yeyote miongoni mwenu anayedhani ana mawazo mazuri juu ya kufanya kitendo cha upendo kwa ufasaha zaidi, waombe wayaseme. Angalia pia mawazo uliyoorodhesha katika somo la 5 "Mungu anataka kanisa kusaidia" na somo la 6 "Kuna mahitaji gani katika jamii tunaweza kusaidia." Kwa pamoja, kubalianeni ni nini mnahisi Mungu anawaongoza kufanya.

Mkisha chagua shughuli, hakikisheni ni kitu mnachoweza kufanya kwa siku moja. Baadhi ya vikundi huchagua vitu vikubwa sana. Tafadhali, endeleeni kuwaza zaidi mpaka mtakapopata kitu ambacho mnaweza kukifanya kwa siku moja, kwa kutumia rasilimali zilizopo na kwa kuwashirikisha watu wengi pia.

Kama mnaweka mipango mkiwa katika vikundi vidogo, waruhusu kila kikundi kushirikisha mawazo yao na wapate mrejesho kutoka kwa washiriki wengine.

- Je, inaonesha Upendo?
- Je, ni ndogo na rahisi?
- Je, inaweza kufanyika kwa rasilimali zilizopo?
- Je, inawashirikisha watu wengi?

Hatua 3: Andika mpango.

Jadili maswali yafuatayo. Kama ikiwezekana, apatikane mtu mmoja wa kuandika majibu mawali haya ili msisahau

- Unaenda kufanya nini?
- Unahitaji rasilimali gani? Utapata wapi vitu hivyo? Nani atavipata?
- Unakwenda kuwasaidia akina nani?
- Nani atashiriki katika kusaidia? Nani atamwalika kila mmoja wenu?
- Tarehe gani utaenda kuufanya?

Maelekezo kwa mwezeshaji: *kama darasa linafanya kazi kaiitka vikundi vidogo, waombe kila kikundi*

wawasilishe mpango wao. Waulize wanakikundi wote kama kuna mapendekezo yoyote yanayoweza kuuboresha mpango zaidi.

Hatua 4: Omba

Ukisha maliza kuandika mpango, Chukua muda wa kuomba tena. Mwombe Mungu akusaidie kukamilisha mradi na kuzidisha zaidi matokeo. Omba kwamba jina lake litatukuzwa. Katika wiki inayofuata au mbili, wakati ukiandaa mradi wako, uwe unaomba ili Mungu akusaidie katika mradi.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *waeleze washiriki kuwa kuna hatua mbili zaidi ambazo hatutazijadili leo. Halafu usome maelekezo ya hatua mbili zilizobaki*

Hatua 5: Fanya mradi

Hatua inayofuata ni kufanya mradi uliopanga. Anza siku kwa maombi na toa jitihada zako kwa Mungu. Kumbuka kwamba unafanya mradi huu kuonyesha upendo wa Mungu kwa jamii yako. Jaribu kuweka mtazamo unaofanana na lengo hili.

Hatua 6: Tathmini na ripoti

Hatua ya mwisho ni kutoa taarifa na kutathmini. Kwa nini tunahitaji kutathmini? Kwa sababu inatusaidia kujifunza. Tunaweza kufikiria kuhusu tulichofanya vizuri na tunachoweza kufanya kuboresha wakati ujao. Haihitaji kuwa mchakato mrefu; Unaweza kuchukua dakika chache kujadili maswali haya:

- Nini kilienda vizuri?
- Nini hakikwenda vizuri?
- Ni maboresho gani tunaweza kuweka kwenye mpango?
- Je, mwitikio ulikuwa kama ulivyokusudia? Kama hapana, kwa nini?
- Je, Mungu alitukuzwa?

Hitimisho

Tumemaliza mtaala wetu wa kwanza! (moduli ya 1)

MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO

Chukua muda kidogo na mjadili katika vikundi vidogo baadhi ya mawazo makuu mnayoyakumbuka katika mafunzo haya.

- Ni jambo gani ambalo unatarajia kulifanya kwa utofauti wiki ijayo?

Tunapohitimisha, tukumbuke habari ya vijana wawili katika Mathayo 21:28-31. Katika hadithi hii kijana mmoja alisema angemtii baba yake lakini hakufanya hivyo. Kijana wa pili alisema asingemtii baba yake, lakini alimtii. Yesu alimsifu yule aliyekuwa mtii. Haitoshi tu kuja hap ana kujifunza, tunatakiwa kuyaweka mafunzo haya katika vitendo. Jamii zetu na Maisha yetu hayatabadilika mpaka pale tutakapoanza kufanyia kazi yale tuliyojifunza. Njia rahisi nia kuanza kwa kuwapenda wengine kupitia kitendo cha upendo au zaidi ya kimoja.

Maelekezo kwa mwezeshaji: *Omba kwa ajili ya washiriki kwamba Mungu atawasaidia kuyafanyia kazi yale yote waliyojifinza.*